SportPesa
TZS. 1,013,643,920
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 8

**MBUNGE** wa Hai atangaza kumaliza chuki na Mbowe



KILIMO CHA MWANI TANZANIA BARA ... Zao jipya linaloshikiliwa na kinamama, shamba lake ndani bahari mikoa Kusini

Ukurasa 12

BUFE

IJUMAA MACHI 11, 2022 Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Jiji Dodoma kuzaliwa upya kupitia ujenzi barabara Km. 112, kuungana kona zote

Ukurasa 14

## Bandari ya Tanga yasukwa upya kukidhi mahitaji soko sasa, yajayo

• Ifikapo Oktoba; kuna gati jipya, kina chaongezwa

**Na Boniface Gideon, TANGA**

TANGA ni kati ya bandari tatu kuu nchini na za kihistoria. Nyinginezo ni Mtwara, pia Dar es Salaam ambayo ni kubwa na maarufu.

Pamoja na umaarufu na ukongwe wake, bandari ya Tanga imekuwa na upungufu katika eneo mojawapo, kwamba haina kina kirefu gatini, hata kuifanya ikapakua mzigo kwa msaada wa matishali, meli zikiegeshwa mbali zaidi.

Hiyo kwa muda mrefu imebaki kuwa kasoro dhidi ya wasifu ilio nao, kwani imechangia sana kuongezeka gharama za upakuaji na upakiaji mizigo kwa wafanyabiashara na wateja wengineo wanaotumia huduma ya bandari.

Ni walakini ambao sasa mamlaka ya kiserikali imeamua kuingilia kati kuitatua kwa kuchimba kina kirefu, sambamba na kuongezeka magati ya kupakua na kupakia mizigo, inayozaa tafsiri kwamba itasaidia kuongezeka idadi ya meli na wateja wanaoitumia.

Kwa ujumla inaelezwa, ni manufaa ambayo mageuzi na ufanisi wa maboresho hayo yanawagusa moja kwa moja watumiaji bandari, kuanzia wenyeji na watokao mikoa jirani kama vile Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

Hali kadhalika, inawagusa wateja wa kigeni waliolazimka hata kufuata huduma hiyo katika nchi jirani, hasa kwa watokao nchi za karibu kama Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Kazi ya ujenzi wa gati la Bandari ya Tanga, ikiendelea. **PICHA: BONIFACE GIDEON.**

Baadhi ya mizigo ya nchi hizo inategemea kupitishiwa bandarini hapo Tanga.Pia, sasa kuna manufaa mapya ya sasa yanajengwa kupitia bomba la mafuta ghafi linaloanzia Hoima nchini Uganda hadi Tanga Chongoleani yote yanatajwa kuongeza uchumi na ajira nyingi kwa vijana.

**ZIARA YA UKAGUZI**

Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), limefanya ziara bandarini Tanga kukagua ufanisi uliopo na mwenyekiti wake, Mussa Mandia, anasema ni aina ya ukaguzi wenye tafsiri pana, hata kugusa bandari ndogo na zilizopewa hadhi 'bubu.'

Kwa ujumla, Mandia anakiri kiridhishwa na kazi ya Upanuzi unaoendelea bandarini, akifafanua: "Tumekuja kutembelea Bandari za Tanga na siyo ya Tanga, kwa kuwa kuna bandari kubwa na bandari ndogo ndogo ambazo ni bubu.

"Tuliwahi kutoa maelekezo TPA (Mamlaka ya Bandari Tanzania) wazirasimishe bandari (bubu), ili kupunguza bandari bubu kwa manufaa ya taifa. Tumeona kwamba kazi inaendelea ya kuboresha Bandari ya Tanga.

"Kwa ajili ya kuimarisha operesheni za bandari kwa maana ya kubeba mizigo mingi na kwa njia ambayo ni salama zaidi, hilo ndilo jambo tunalosimamia pamoja na utendaji wa bandari" anaeleza Mandia

Pia, anakiri ameona kina cha bandari kinaongezwa kufikia mita 13, jambo litaloiwezesha meli kufika mpaka bandarini

Anasema, kinachofanyika sasa ni kuongeza kina cha bandari kutoka mita tatu hadi 13, jambo litaloziwezesha meli kuingia bandarini, tofauti na zamani operesheni ilifanyika katikati ya maji.

Mandia anaeleza matarajio ni baada ya ujenzi huo kukamilika mwezi Oktoba mwaka huu, meli kubwa zitatia nanga kwenye gati jpya, matarajio ni kwamba italeta tija katika upana wake, ikijumuisha usalama wa watu na mizigo inayopakuliwa na kupakiwa, huku pia ikiongezeka.

**WASIMAMIZI BANDARI**

Meneja wa Bandari ya Tanga, Masudi Mrisha, anasema ujenzi wa gati hizo utakapokamilika, ...

utakua umekamilika na meli zenye urefu huo zitaweza kuingia bandarini na mpaka mwezi Oktoba, mita zote 450 zitakuwa zimekamilika."

Meneja huyo anaeleza kuwa ana matarajio baada ya kukamilika upanuzi, meli za aina mbalimbali zitaweza kuwasili bandarini hapo na kupakua mizigo kufikia tani zaidi ya milioni tatu kwa mwaka.

"Magari yataweza kuwasili na kushusha mizigo hapa, mizigo itaongezeka na shehena zitakazokuwa zinawasili zitapakuliwa kwa haraka," anasema Mrisha na kuongeza:

"Kwa sasa bandari inahudumia tani 71 8,400. Kukamilika kwa gati hizo mbili, bandari itaweza kuhudumia mzigo wa tani milioni tatu," anasema Meneja wa Bandari.

**WANA TANGA WANENA**

Abdalah Saleh, ni mkazi anayepata mkate wa kila siku katika shughuli za ujenzi huo, ana maoni kadhaa alipohojiwa na Nipashe, kwamba: "...ujenzi huu tumejipatia kazi, mwanzo tulikaa tu maskani tukiwa hatuna kazi, lakini leo hii tunashukuru mkono unaenda kinywani miezi zaidi ya minne."

Mwanamkasi Mwandorwa, anayeuza vyakula na vinywaji eneo la Bandari, naye ana neno lake kuwa: "Wametuletea Neema kubwa hasa kwa sisi kina mama ambao tunajishughulisha na biashara za vyakula.

"Mimi sasa hivi nina uwezo wa kuuza 'vi-ndoo' vitatu vya ubwabwa, wakati mwanzo nili-...

UKURASA 11

Ijumaa Machi 11, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580881
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



## VITA UKRAINE

# Mtanzania aliyenusurika asimulia yote yaliyomkuta

**ASEMA** ni mwendo wa makombora, hakuna kulala...

*Endelea ukurasa 4*



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akifanyiwa maombi maalum na viongozi wa kimila wa Wamasai 'Laigwanan', kabla ya kuzungumza nao, kwenye viwanja vya Chuo cha Ufundi Arusha, jana. **PICHA: OWM**

# Polisi yamtaka Makonda kufuata sheria na taratibu

UKURASA 2



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro



Paul Makonda

## Hofu yatanda vifo vya samaki katika Mto Mara

UKURASA 2

UKURASA WA 3

### BIDHAA MUHIMU KUADIMIKA SABABU VITA VYA UKRAINE

WAZIRI wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, amesema...

UKURASA WA 3

### ZIARA YA RAIS SAMIA UBELGIJI YALETA BIL. 62/-

SERIKALI ya Ubelgiji imeahidi kuipatia Tanzania Euro milioni 25 sawa na shilingi za Tanzania bilioni 62...



UKURASA WA 19

### FISI ALIVYOMJERUHI MWANAFUNZI KICHWANI

MWANAFUNZI wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Somanda "A", Halmashauri ya Mji wa Bariadi mkoani Simiyu, Hollo Malugu (14), ameng'atwa...

**MICHEZO** MAKALLA: TWENDENI NA SIMBA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Polisi yamtaka Makonda afuate sheria na taratibu

Na Mwandishi Wetu

KAMANDA wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, amesema Jeshi la Polisi halijapokea malalamiko yoyote kutoka kwa aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kuhusu madai ya kutishwa kupigwa risasi.

Jana, kwenye mitandao ya kijamii kulisambazwa video fupi ikimwonyesha Makonda akilalamikia alichokiita kupokwa eneo mkoani Dar es Salaam huku kukiwa na madai kwamba ametishiwa kupigwa risasi.

Alipotafutwa na Nipashe kuzungumzia suala hilo, Kamanda Muliro alisisitiza kufuatwa kwa utaratibu uliowekwa kisheria kushughulikia jinai nchini.

"(Makonda) ametishiwa na nani? Mtu akitishiwa si anakwenda kituo cha polisi? Mwambie 'tupe namba ya kesi uliyoishtaki inayochunguzwa polisi'. Mashtaka hayafunguliwi kwenye mitandao," alisema.

Kamanda Muliro alisisitiza kuwa mashtaka yoyote yanayotakiwa kuchunguzwa na Jeshi la Polisi, hayafunguliwi kwenye mitandao ya kijamii bali kwenye vituo vya polisi.

"Vituo vya polisi vifungwe ili vibaki kwenye mitandao kama anavyoripoti kwenye mitandao?" Kamanda Muliro alihoji.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (katikati), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. bilioni 2.2 kwa Muhamed Suleiman Khamis, jijini Zanzibar jana, kwa niaba ya wananchi wenzake, kwa ajili ya fidia ya waliohamishwa eneo la Red Zone, kupisha ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tunguu, Mkoa wa Kusini Unguja. **Habari Uk. 17. PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# PM apokea majina ya walio tayari kuhama Ngorongoro

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amepokea orodha ya majina ya awali ya kaya 86 zenye watu 453 ambao wamekubali kuondoka kwenye Hifadhi ya Ngorongoro kwa hiari huku wengine wakiendelea kujiandikisha.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa mazungumzo ambayo Waziri Mkuu aliyafanya na wadau wa uhifadhi kwenye vikao vilivyofanyika Februari 14 na 17, mwaka huu, kwenye tarafa za Loliondo na Ngorongoro, wilayani Ngorongoro, mkoani Arusha.

Waziri Mkuu alipokea majina hayo jana baada ya kumaliza kikao na viongozi wa kimila wa jamii ya Kimasai (Laigwanan) kwenye mkutano uliofanyika eneo la Oretei Loongaik - Marya, kwenye Chuo cha Ufundi Arusha, jijini Arusha. Eneo hilo hufanyika Bunge la viongozi hao na hutumika pia kufanyia ibada za kimila.

Akikabidhi orodha hiyo kwa Waziri Mkuu, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, alisema majina hayo ni ya awali na tayari yalishahakikiwa baada ya wakazi hao kujiandikisha.

Akizungumza na Malaigwanan hao zaidi ya 350, Majaliwa alisema Rais Samia Suluhu Hassan alipofanya ziara mkoani humo aliliambia taifa iko hatari ya kutoweka kwa hifadhi ya Ngorongoro ndani ya muda mfupi na akatoa maagizo viongozi waende kuwasikiliza wananchi juu ya hatua za kuchukua ili tunu hiyo isipotee.

"Ile hatari aliyosema Mheshimiwa Rais ni ipi? Zamani watu waliishi na wanyama bila tatizo kwa sababu kulikuwa na wakazi 8,000 tu wenye ng'ombe 20 hadi 30. Leo hii kuna wakazi 110,000 na zaidi ya mifugo 813,000 wakiwemo ng'ombe, mbuzi na kondoo.

"Zamani maboma yalikuwa yamesambaa lakini leo hii nyumba zimejaa, tena za bati na matofali. Idadi ya watu imeongezeka, idadi ya mifugo imeongezeka na makazi yameongezeka. Hakuna huduma za afya au shule wakati ni hitaji muhimu kwa wananchi," alisema.

Majaliwa aliwaeleza viongozi hao kwamba serikali imetenga eneo la kilometa za mraba 400,000 wilayani Handeni ambalo kati ya hizo, kilometa za mraba 220,000 zilitumika kwa kujenga nyumba, kupima viwanja na kutenga maeneo ya malisho.

Majaliwa aliwaeleza viongozi hao wa kimila kwamba Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia eneo lao la kufanyia ibada za kimila liendelee kutumika kwa sababu ni jambo jema.

Mapema, Kiongozi Mkuu wa Jamii ya Wamasai Tanzania, Isack Ole Kisongo, alisema kwa nafasi yao viongozi wa kimila wako tayari kushirikiana na serikali kuhakikisha rasilimali za nchi zinawanufaisha Watanzania wote.

Alisema suala la kuhama Ngorongoro halina tofauti na maeneo mengine ambako wananchi waliondoka kwa amani kupisha miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa reli ya kisasa, bomba la mafuta la kutoka Tanga hadi Uganda na ukuta wa Mererani.

# Hofu yatanda vifo samaki Mto Mara

Na Richard Makore, MUSOMA

HOFU imetanda katika baadhi ya vijiji vinavyopakana na Mto Mara ambao unamwaga maji yake Ziwa Victoria baada ya samaki aina ya sato kuonekana wakielea huku wakiwa wamekufa.

Samaki hao walianza kuonekana Machi 8, mwaka huu, huku maji ya mto huo yakionekana kuwa na rangi nyeusi na juu kukiwa kumetanda kitu kinachoonekana kama mafuta.

Habari kutoka katika vijiji hivyo zinasema kwa sasa wananchi ambao wanatumia maji hayo kwa ajili ya kunywa, kunyweshea mifugo na kufanya shughuli za uvuvi, wameingiwa na hofu.

Licha ya samaki hao kufa, baadhi ya wananchi wametumia fursa hiyo na kuingia mtoni na kuwaokota kisha kuwauza kwa wananchi kwa bei rahisi.

Vijiji vilivyokumbwa na tatizo hilo ni Kuruya, Kwibuse na Marasibora na kwamba maji hayo yaliyochufuliwa yanaingia katika Ziwa Victoria, jambo ambalo linaweza kusababisha samaki zaidi kufa ziwani.

Mmoja wa wananchi wa kijiji cha Kuruya ambacho kinapakana na mto huo, Odhiambo Musa, alisema maji hayo yanatoa harufu na yamekuwa na utando wa kitu kama mafuta kwa juu na kwamba watu wanaendelea kuokota samaki hao na kuwatumia kama kitoweo na wengine kuwauza.

Alisema baadhi ya wananchi wamejaribu kuwakataza wenzao kutumia samaki hao lakini hawaelewi badala yake wanaendelea kuwala.

Ofisa Habari wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Victoria (LVBWB), ambalo linasimamia rasilimali za maji katika Kanda ya Ziwa, Perpetua Masaga, alikiri maji ya mto huo kuchafuliwa.

Alisema wamechukua sampuli na kuzipeleka katika maabara yao kwa ajili ya kupima ili kujua nini kimetokea katika mto huo na kusababisha samaki kufa.

"Ni kweli samaki wamekufa na tayari tumechukua sampuli za maji ili kuyapima kuona kama yamechafuliwa na binadamu au ni mabadiliko ya hali ya hewa," alisema.

Masaga alisema wanafanya kazi hiyo kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI).

Ofisa huyo alisema uchafuzi huo wa mazingira umelikumba eneo la daraja la Kirumi na kwamba uchunguzi wa maabara ukikamilika watatoa taarifa kwa umma.

Akizungumzia na Nipashe jana kuhusu hali hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Rashid Tamutamu, alikiri kupatiwa taarifa hiyo na kwamba ameiagiza TAFIRI kuchukua sampuli za samaki hao ili kwenda kuwapima katika maabara ya usalama wa chakula mjini Musoma.

Alisema tayari uchunguzi huo umeanza na kwamba kazi hiyo inaweza kukamilika baada ya siku mbili na kuahidi kufuatilia kwa karibu suala hilo.

Mwaka jana, samaki aina ya sangara walionekana katika Ziwa Victoria wakiwa wamekufa na kuzua taharuki kwa baadhi ya wakazi wa Kanda ya Ziwa.

Hata hivyo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia wataalamu wake, ilitoa taarifa kwamba vifo vya samaki hao vilitokana na mabadiliko ya hali ya hewa ndani ya ziwa.

## HABARI KITAIFA



Naibu Spika, Mussa Azan Zungu, akisalimiana na wadau wa samaki wa Soko la Feri, katika mkutano mkuu wa pili wa mwaka uliofanyika jijini Dar es Salaam jana kujadili mambo mbalimbali sokoni hapo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Bidhaa muhimu kuadimika sababu ya vita vya Ukraine

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, amesema Tanzania itaathirika kiuchumi kutokana na vita vinayoendelea nchini Ukraine.

Amesema Tanzania imekuwa ikipeleka mazao ya biashara kama chai, kahawa na mazao ya uvuvi pamoja na vito vya thamani yakiwamo madini ya Tanzanite na dhahabu.

Dk. Kijaji alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari hukusu mafanikio ya mwaka mmoja wa Rais Samia katika sekta za uwekezaji, viwanda na biashara.

Alisema kitendo cha Russia kuivamia Ukraine, kinasababisha pia bidhaa zilizokuwa zinatoka nchini humo kusitishwa kuingia nchini zikiwamo ngano na mitambo ya viwanda.

"Kwanza tulikuwa tunapeleka wanafunzi kwenda kupata elimu na tumefanikiwa wametoka salama wote. Wanafunzi wetu walikuwa wanapikwa katika maeneo maalum," alisema.

Alitaja eneo lingine litakaloathirika kuwa ni utalii ambako watalii walikuwa wakitembelea vivutio mbalimbali nchini. Alisema kwa wakati huu vita vikiendelea, biashara itasimama na kuathiri uchumi wa mataifa mengine ambayo wanashirikiana na Ukraine.

"Huwezi kufanya biashara na mtu ambaye hajatulia. Kwa hiyo tutapata madhara katika bidhaa ambazo tulikuwa tunapeleka na ambazo tulikuwa tunachukua kutoka kule," alisema Dk. Kijaji.

Pia alisema Rais Samia Suluhu Hassan alishasema kinachoendelea nchini, kupanda kwa bei za bidhaa ni matokeo ya vita hivyo vinayoendelea nchini Ukraine.

"Tunapaswa kuziombea nchi hizi kusitisha mapigano yanayoendelea ili kurejea katika hali yake ya amani," alisema.

Kwa takribani wiki mbili sasa, majeshi ya Russia yamekuwa yakiishambulia Ukraine huku watu kadhaa wakiripotiwa kupoteza maisha, wengine kujeruhiwa na kukimbia makazi yao kwenda nje ya mipaka ya nchi hiyo.

# Ziara ya Samia Ubelgiji yaleta bil. 62/-

**Na Benny Mwaipaja,** DODOMA

SERIKALI ya Ubelgiji imeahidi kuipatia Tanzania Euro milioni 25 sawa na shilingi za Tanzania bilioni 62, kwa ajili ya kutekeleza programu mpya ya maendeleo ya miaka mitano katika sekta ya elimu, inayotarajiwa kutekelezwa kuanzia mwaka 2023 hadi mwaka 2027, katika mkoa wa Kigoma.

Ahadi hiyo ilitolewa jijini Dodoma na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Ubelgiji-ENABEL, Koenrad Goekint, aliyeongoza ujumbe wa watu 7 kutoka nchini Ubelgiji walipokutana na kufanya mazungumzo na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango ambaye ni Mlipaji Mkuu wa Serikali, Emmanuel Tutuba.

Goekint alisema kuwa programu hiyo itajikita katika kuendeleza sekta ya elimu kwa kuangazia maeneo ya ukuzaji ujuzi wa ajira na utaalamu kwa vijana hususani masuala ya uanagezi na ujasiriamali, kwa lengo la kuzalisha ajira, kuimarisha usawa wa kijinsia kwa kukuza zaidi ushiriki wa wanawake kwenye shughuli za maendeleo na kuboresha masuala ya usawa wa kijinsia.

Tutuba, aliishukuru ENABEL kwa kuja na programu hiyo itakayotoa matokeo mazuri kwa kugusa maisha ya wananchi wa Tanzania katika kuwaletea maendeleo.

"Programu hii itakayotekelezwa mkoani Kigoma itagusa maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa kwenye utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26), wenye lengo la kuboresha huduma za jamii, maisha ya watu na elimu ni moja ya maeneo hayo," alisema Tutuba.

Tutuba aliiomba Serikali ya Ubelgiji kupitia ENABEL, kuangalia uwezekano wa kuongeza maeneo mengine ya kimkakati ya kuboresha maisha ya wananchi ikiwamo huduma za afya na maji kwani wanawake ndio walengwa wakuu na ndio wanaokabiliana na changamoto ya uhaba wa maji. Aidha, Tutuba aliishauri Serikali ya Ubelgiji kupitia shirika hilo kutekeleza mradi kama huo kwa upande wa Zanzibar ili kuwawezesha wananchi wa Visiwa hivyo kufurahia matunda mazuri ya uhusiano mwema uliopo kati ya Tanzania na Ubelgiji.

Balozi wa Tanzania nchini Ubelgiji, Jestas Nyamanga, alisema kufanyika kwa ziara hii ni ishara nzuri ya kuendelea kuimarika kwa uhusiano wa kimaendeleo kati ya Tanzania na Ubelgiji na ni matokeo chanya ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan, alipofanya ziara ya kikazi nchini Ubelgiji Februari 14 hadi 19 mwaka huu.

Akiwa Ubelgiji, Rais alikutana kwa mazungumzo na viongozi mbalimbali akiwamo Alexander De Croo, Waziri Mkuu wa Ubelgiji ambapo viongozi hao walikubaliana kuweka mikakati ya kufanyika kwa majadiliano ya programu ya maendeleo na kuhakikisha kuwa mchakato wa maandalizi unakamilishwa kwa wakati.

Balozi Nyamanga alifafanua kuwa Tanzania imeingia katika orodha ya nchi 15 pekee duniani ambazo Ubelgiji inaendesha program kama hizo jambo ambalo ni ishara ya mafanikio makubwa ya uhusiano uliopo kati ya nchi hizi mbili na alitoa wito kwa taasisi zote zitakazo kutana na ujumbe huo wa Ubelgiji nchini kuweka kipaumbele mahitaji ya nchi katika eneo husika.

Ujumbe wa ENABEL unajumuisha watu saba na upo nchini kuanzia Machi 7 hadi 18, 2022, ambapo watafanya mazungumzo na viongozi mbalimbali wa Wizara na Taasisi za Serikali kuhusu maandalizi ya programu mpya ya ushirikiano.


## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## TANGAZO KWA WADAIWA WA VIWANJA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia Wananchi wote wanaodaiwa viwanja katika maeneo ya Mtumba, Michese, Nzuguni, Kitelela, Kikombo, Iyumbu, Nzuguni Bus Stand, Nala Industrial Area, Njedengwa Investment Area, Nala, Chahwa, Iyumbu New Town Centre, Mahomanyika, Vikonje, Nala-Chigongwe, Ihumwa, Mapinduzi, Medeli, Nala-Lugala na Nala-Segu kuwa muda wao wa kulipia viwanja hivyo umeisha. Aidha, katika kuwawezesha kukamilisha malipo hayo, amewaongezea muda hadi tarehe 27.03.2022.

Baada ya kukamilika kwa muda huo, viwanja ambavyo vitakuwa bado vinadaiwa vitarudishwa sokoni ili wateja wengine wavinunue bila kutoa taarifa yeyote kwa mteja wa awali.

**Tangazo hili limetolewa na:**
**Mkurugenzi wa Jiji, DODOMA**

216731401

MAKALA MAALUM

VITA UKRAINE

# Mtanzania aliyenusurika asimulia yaliyomkuta

- Yeye na wenzake waokolewa na Shirika la Msalaba Mwekundu



Wanafunzi Watanzania waliofanikiwa kuondoka Ukraine. **PICHA: MTANDAO**

**Na Salome Kitomari**

"KATI ya vitu ambavyo sitosahau ni siku tuliyokuwa tumelala majira ya saa moja usiku, baada ya vita kuanza tulikuwa tunatakiwa kuzima taa. Lilirushwa kombora kwenye kituo cha kuzalisha umeme jirani na jengo kuu la chuo chetu cha Sumy (Poltavo, Ukraine).

"Lilisababisha tetemeko kubwa sana na mwanga kutoka angani, tukahisi ni radi bila mvua. Hadi sasa nikikaa mwenyewe, hali ile inanisumbua akilini," mmoja wa wanafunzi manusura 32 wa Kitanzania walioondolewa kwenye ukanda huo wa janga, ameisimulia Nipashe.

Katika mazungumzo na Nipashe jana, mwanafunzi huyo wa kiume (jina tunalihifadhi), aliendelea kusimulia kilichojiri, akitamka:

"Kulikuwa na fununu kwamba kuna wadunguaji walikuwapo, hivyo muda wote wa usiku tunazima taa. Walivyopiga kombora, umeme ulikatika mji mzima, wote tulikimbilia basement (ghorofa ya chini).

"Tangu kuzaliwa kwangu sijawahi kuona wala kusikia mtetemo mkubwa kama huo kwa sababu nimezaliwa na kukua kwenye nchi yenye amani Tanzania, ilinisumbua sana, hadi sasa imeshindwa kuondoka kwenye kichwa changu, nikikumbuka nakosa amani kabisa."

> "Kuna wakati ilibidi kubadilisha gari baada ya kuharibika kiasi cha kushindwa kuendelea na safari, safari ilichosha

Mwanafunzi huyo alisema kuwa baada ya kuanza kwa vita hivyo, walitakiwa kuzima taa wanapokuwa ndani kwa kuwa kulikuwa na majibishano ya risasi, hivyo ingewezekana kupigwa kwa kuhisi ni adui.

Alisema kuwa jana mchana walikuwa wamefika eneo salama na mpango uliokuwapo ni kuwapeleka ama Hungary au Poland na hawakujua wa kuwapokea, lakini wanajua kuna utaratibu umeandaliwa kuhakikisha wote wanapokewa.

"Tuliondoka na vitu vidogo kama nguo, viatu vichache, chakula kama mikate, biskuti na maji ambavyo kila mmoja aliweka kwenye begi dogo linalobebeka kiurahisi. Mali zetu zingine zote tumeziacha chuoni," alisema alipoulizwa na Nipashe kama walifanikiwa kunusuru mali zao.

Alisema safari ya kutoka Sumy ilikuwa ndefu sana kwa kuwa walitoka huko saa saba mchana na kufika siku ya pili saa nne usiku, wakiwa kwenye msafara wa mabasi na baadaye treni.

"Tulinunua vyakula Sumy wakati tunatoka, tulikula tukiwa kwenye treni, wakati tukiwa kwenye treni, kuna mama mmoja alijitolea kugawa biskuti na maji kwa abiria, nasi tulipewa hadi tunafika hapa," alisema.

Mwanafunzi huyo alisema wanamshukuru Mungu wote waliokuwa wamebaki chuoni huko wana afya njema na wamefanikiwa kuvuka mpaka.

Alisema waliondolewa nchini humo kwa msaada wa Shirika la Msalaba Mwekundu ambalo lilifika chuoni huko kuwaondoa wanafunzi wote wa kigeni, wanawake na watoto wakapelekwa Mji wa Poltava.

"Tulisafiri kwa zaidi ya saa sita kwa basi, tukapanda treni kwa saa tisa hadi kufika Mji wa Kyiv na baadaye wakafika Lviv saa nne usiku. Leo (jana) tunakwenda Hungary na baadhi watakwenda Poland ndipo tuanze safari ya kurejea nyumbani Tanzania," alisema.

**SAFARI ILIVYOKUWA**

Mwanafunzi huyo anaendelea kusimulia kilichojiri wakati wa safari yao hiyo, akiwasilisha: "Safari ilikuwa ni ndefu sana ya magari mengi, watu wanakimbia Sumy kwenda Poltava, tulichoka sana, baridi kali sana wakati mwingine gari liliharibika njiani, inabidi tushuke tusukume licha ya hali ya baridi kali sana.

"Kuna wakati ilibidi kubadilisha gari baada ya kuharibika kiasi cha kushindwa kuendelea na safari, safari ilichosha sana.

"Tulisafiri kupitia vijijini, tulifika kituo cha treni cha Poltava saa nane unusu usiku tukajikusanya Watanzania wote pamoja, tukapanda treni kwa saa nyingi hadi Kiev ambako tulifika saa nne usiku.

"Hatukubaguliwa, wote tulipanda treni na wazungu, haikuwa ya kugombania, wote tulikaa kwenye viti kwa nafasi, njiani tulikuwa tunakutana na vifaru vya jeshi vinatoka Magharibi kwenda Mashariki Ukraine.

"Kwa kweli tuliogopa sana, treni haikuwa inakimbia kwa mwendo mkali, hivyo safari ilichukua muda mrefu sana, tulipofika tulipokelewa na kupata sehemu ya kulala."

**KURUDI TANZANIA**

Mwanafunzi huyo alisema kuwa baada ya kufika eneo hilo, kilichokuwa kinaendelea jana ni kukamilisha taratibu za kusafiri kwenda Hungary na Poland ambako watatumiwa fedha na wazazi wao ili wakate tiketi za kurejea Tanzania.

"Kusafiri kutoka Hungary au Poland hadi Tanzania kila mzazi inabidi atoe fedha kumsafirisha mwanawe. Wenzetu wote waliofanikiwa kufika huko (Tanzania) walitumiwa fedha na wazazi wao, wakakata tiketi na kusafiri hadi nyumbani," alisema.

Kuhusu taaluma, mwanafunzi huyo alisema wako wanafunzi mchanganyiko waliokuwa wameanza masomo na vita vimetokea wakiwa mwishoni mwa muhula wa kwanza; walioko muhula wa pili na wanaochukua shahada ya uzamili ambao wana miaka mitano huko.

"Wengi walikuwa mwaka wa kwanza na wa pili. Mimi nilikuwa nimemaliza muhula wa kwanza. Nilikuwa ninakaribia kufanya mtihani ili niingie muhula mwingine, ila nimeshindwa kutokana na vita," alisema.

**NASAHA KWA WATANZANIA**

Mwanafunzi huyo alisema amejifunza kuwa vita siyo jambo zuri na halipaswi kushabikiwa kwa kuwa wanaoteseka ni wengi na uharibifu mkubwa wa mali unatokea.

Kijana huyo alisisitiza kuwa hakuwahi kutarajia kushuhudia kilichowakuta masomoni Ukraine kwa kuwa amekulia Tanzania kwenye amani.

"Kama kuna watu wamekaa wanafikiri kuhusu vita, waache kabisa! Unakuwa katika maisha ya hofu muda wote, wakati tupo Sumy unasikia wamepiga mji fulani, kutoka chuoni hadi mpaka wa Urusi ni dakika 45, unaishi unawaza muda wowote watawapiga, unaishi kwa woga na wasiwasi mkubwa," alisema.

"Ilifika mahali tunakosa huduma za kijamii kama umeme na maji, dawa zinaisha, kupata fedha ni ngumu kwa kuwa kwenye ATM kuna watu wengi, inaharibu mfumo wa maisha na masomo, tulitakiwa kufanya mitihani ya muhula lakini imeshindikana.

"Vita siyo nzuri, fedha ambazo zingewekezwa kwenye huduma za kijamii zimeelekezwa kwenye vita, muda wa maendeleo unaelekezwa kwenye vita. Naomba dunia ishawishi amani na siyo vita. Kama kuna mtu anapenda vita atuulize sisi tuliopitia haya maisha kwa siku kadhaa," alihitimisha.

Kijana huyo ni miongoni mwa wanafunzi 32 ambao Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilisema juzi kuwa ni kundi la mwisho la waliokuwa wamekwama Ukraine.

Kwa mujibu wa wizara hiyo, kundi hilo liliondolewa kwa mabasi hadi Poltavo na Lviv kwa lengo la kuingia Hungary na Poland.

## HABARI KITAIFA

# Kesi ya Sabaya yakwama kisa majukumu ya hakimu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha imeahirisha kuendelea kusikiliza kesi ya uhujumu uchumi namba 27 inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya na wenzake sita kwa kuwa hakimu anayeisikiliza amekwenda kwenye majukumu mengine ya kiofisi.

Kesi hiyo ilipangwa kuendelea kusikilizwa jana mahakamani huko kwa shahidi wa tano wa utetezi, Jackson Macha, kuendelea kutoa ushahidi, akiongozwa na Wakili wake, Edmund Ngemela.

Akiahirisha shauri hilo jana, Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Pamela Meena, alisema Hakimu Dk. Patricia Kisinda aliyekuwa anasikiliza kesi hiyo amepata udhuru na atakuwa kwenye majukumu mengine ya kiofisi.

Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Watson Mwahomange, Silvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31), wanaokabiliwa na mashtaka matano yakiwamo ya matumizi mabaya ya madaraka, kuongoza genge la uhalifu, kujihusisha na vitendo vya rushwa na utakatishaji wa fedha.

"Ninaahirisha kesi hii hadi Machi 14, 2022 kwa kuwa hakimu anayesikiliza shauri hili yupo kwenye majukumu mengine ya kikazi," alisema Hakimu Pamela.

Awali Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ofmedy Mtenga, alidai kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa.

Katika kesi hiyo, shtaka la kwanza ni kuongoza genge la uhalifu linalowakabili washtakiwa wote. La pili ni kujihusisha na vitendo vya rushwa na linalomkabili mshtakiwa wa kwanza Ole Sabaya.

**Jordan University College**
Office of the Deputy Principal Finance and Administration
Constituent College of St. Augustine University of Tanzania
P.O. Box 1878, Morogoro, Tanzania,
Email: dpfa@juco.ac.tz; Website: www.juco.ac.tz

**Ref: HR/VA/2022/01** **10 March 2022**

## VACANCIES ANNOUNCEMENT

- **Position: Lecturer / Senior Lecturer**
  1. Education on Planning and Administration (1)
  2. Law (2)
  3. Sociology (1)
  4. Accounting and Finance (2)
  5. Marketing (1)
  6. ICT (1)
  7. Psychology and Counselling (1)

**Reports to the Head of Department**

**Duties**

- Teaching in formal courses and seminars, undertaking individual research and participating in bigger multidisciplinary research projects; preparing manuals, simulations and case studies for training; provide close supervision and guidance to students; working on consultancy projects; coaching junior teaching/research staff and any other duties as may be assigned to him/her by his/her reporting officer.

**Requirements:**

A PhD in relevant field with Masters and Bachelor degree in the relevant field with a minimum GPA of 4.0 and 3.5 respectively.

- **Position: Assistant Lecturer**
  1. Education on Planning and Administration (1)
  2. Law (1)
  3. Sociology (1)
  4. Marketing (1)
  5. Library Records and Archive Management (1)
  6. ICT (1)
  7. Psychology and Counselling (1)

**Reports to the Head of Department**

**Duties**

- With guidance of senior staff members conduct lectures, research and consultancy projects, tutorials, seminars, marking tests, assignments, examinations and submitting results of the same timely. Preparing case studies and any other duties as may be assigned to him/her by his/her supervisor

**Requirements:**

A consistence of Masters and Bachelor degree in the relevant field with minimum GPA of 4.0 and 3.5 respectively.

**Application Instructions:**

Send your application consisting of a cover letter indicating the position you are applying for in the SUBJECT email, CV in English and Copies of Academic Certificates and transcripts through the following address not later than 16 March 2022. You are encouraged to send your application electronically through the given email.

**Deputy Principal for Finance and Administration, Jordan University College,**
**P. O. Box 1878, Morogoro-Tanzania**
**E-mail: dpfa@juco.ac.tz**
**Cc: hro@juco.ac.tz**

**N.B.** Only shortlisted candidates will be contacted.

MEDIA COUNCIL OF TANZANIA

## UAMUZI WA KAMATI YA MAADILI YA BARAZA LA HABARI TANZANIA (MCT)

Lalamiko Namba 2/2021
Mohammed Enterprises Tanzania Limited (METL) (Mlalamikaji)
Na
Gazeti la Jamhuri (Mlalamikiwa)
Tarehe ya Kikao: 24Februari, 2022
Mahali pa Kikao: Ukumbi wa Mikutano wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Kijitonyama, Dar es Salaam

Akidi: Mhe. Jaji (Mstaafu) Robert V. Makaramba – Mwenyekiti
Bi. Edda Sanga – Makamu Mwenyekiti
Bi. Anna Henga – Mjumbe
Bw. Happines Nkya – Mjumbe
Dk. Joyce Bazira – Mjumbe
Bw. Kajubi Mukajanga – Katibu wa Kamati
Mlalamikaji: METL akiwakilishwa na:
Bi. Neema Mahunga – Wakili
Bi. Zakhia Ali– Company Secretary
Mlalamikiwa: Gazeti la Jamhuri likiwakilishwa na:
Bw. Manyerere Jackton Nyerere – Naibu Mhariri Mtendaji

Mwenyekiti alifungua kikao cha usuluhishi kwa kuwakaribisha wasuluhishi kutaja kama kwanza, wana mgongano wowote wa maslahi katika lalamiko hilo. Alianza kwa kusema yeye mwenyewe ndie alikuwa Jaji aliyesikiliza kesi inayotajwa ndani ya habari inayolalamikiwa, wakati huo akiwa katika Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara, na akataka Mlalamikaji na Mlalamikiwa waseme kama wako radhi aendeshe kikao hicho cha usuluhishi. Wote, Mlalamikaji na Mlalamikiwa, walitoa ridhaa yao kuwa walikuwa radhi, Mhe Jaji Mstaafu Robert V. Makaramba aendeshe kikao hicho.

Hapakuwa na suala jingine la uwezekano wa mgongano lililotajwa.

Jambo la pili lilikuwa kutazama uhalali wa Kamati ya Maadili ya Baraza la Habari Tanzania ambacho ndicho chombo kinachoendesha usuluhishi huo. Mwenyekiti alitanabahisha kuwa chombo hicho kinapata uhalali wake kwenye kifungu cha 3(c) cha Katiba ya Baraza la Habari Tanzania (MCT).

Jambo la tatu lilikuwa washiriki katika usuluhishi huo kukubali wenyewe kwa ridhaa yao kusuluhishwa na kukubali kuwa maamuzi yatakayofikiwa yatawabana na watayatekeleza. Wote, Mlalamikaji na Mlalamikiwa walikubali na kusaini fomu maalum kuonyesha ridhaa yao.

Jambo la nne ilikuwa kwa Mwenyekiti kuwakumbusha washiriki katika usuluhishi huo pamoja na Wajumbe wa Kamati umuhimu wa kuzingatia usiri katika mashauri ya usuluhishi. Kwa sababu hiyo, Mwenyekiti aliwasimamisha watu wasio wajumbe wa Kamati waliokuwamo ukumbini na kuwataka wajitambulishe, kisha akawauliza Mlalamikaji na Mlalamikiwa kama walikuwa radhi watu hao waendelee kuwamo ukumbuni wakati usuluhishi ukiendelea. Watu hao walikuwa waandishi na maafisa wa MCT. Wote, Mlalamikaji na Mlalamikiwa, walitoa ridhaa yao.

Jambo la tano, Mwenyekiti alitoa mwongozo wa utaratibu wa kuendesha usuluhishi huo kwamba: washiriki na Wajumbe wa Kamati kukubaliana juu ya mambo yanayobishaniwa; Mlalamikaji ndie ataanza kutoa maelezo yake, kisha atafuatiwa na Mlalamikiwa ambaye naye atatoa maelezo ya upande wake, na hatimaye Mlalamikaji atajibu. Kisha Wajumbe wa Kamati watashauriana na kutoa uamuzi na kuhitimisha usuluhishi.

Baada ya hapo Mwenyekiti alikiongoza kikao cha usuluhishi kukubaliana mambo yanayobishaniwa ambayo yataangaliwa katika mchakato huo wa usuluhishi.

**Kikao kilikubaliana kwamba mambo yanayobishaniwa ni:**

1. Kwamba makala inayolalamikiwa iliichafua kampuni ya METL na viongozi wake wa juu kwa kuwatuhumu kwa mambo yasiyokuwa kweli;
2. Kwamba gazeti la Jamhuri lilichapisha makala ya upande mmoja bila kuwatafuta walalamikaji na kusikia upande wao na hivyo kukiuka msingi muhimu wa maadili ya taaluma ya uandishi wa habari.

### Maelezo ya Mlalamikaji kwa kifupi

Mlalamikaji alitoa maelezo ya malalamiko yake akirejea mawasiliano yake na MCT pamoja na vielelezo vikiwamo nakala ya makala inayolalamikiwa iliyochapishwa katika toleo Na. 497 la Aprili 6 – 12, 2021 yenye kichwa cha habari: Matajiri 'waumana' kwa kinu cha NMC.

Wakili Neema Mahunga kwa niaba ya Mlalamikaji aliorodhesha hitilafu kadhaa katika makala hiyo zikiwamo kutajwa kwa majina ya watu katika mambo ambayo hawakuhusika. Watu hao walikuwa Gulam Abbas Dewji – Mwenyekiti wa Kampuni ya METL, Mohammed Dewji – Mtendaji Mkuu wa METL, na Hussein Hassanali (Hussein Dewji) – Mkurugenzi wa Manunuzi.

Kati ya mambo aliyokanusha, Mlalamikaji alisema sio kweli kwamba Gulam Dewji aliichongea kampuni ya Monaban kwa TAKUKURU wala TRA; sio kweli kwamba Gulam Dewji alimtishia mmiliki wa Monaban (Mollel); Mohammed Dewji hajawahi kushiriki katika vikao vinavyotajwa katika habari inayolalamikiwa; sio kweli kwamba maafisa wakuu wa METL waliwahi kuomba au kudai asilimia 60% ya hisa za kinu tajwa; wala Gulam Dewji hajawahi kufungua kesi yoyote kuhusu kinu hicho kama inavyotajwa na Mlalamikiwa.

Mlalamikaji alisema kama Mlalamikiwa angefanya jitihada za kuongea na walalamikaji angepata ukweli kabla ya kuchapisha makala hiyo.

Mlalamikaji alisema kwa sababu hiyo wanaomba nafuu zifuatazo:

1. Mlalamikiwa aombe radhi mara tatu katika matoleo ya gazeti la Jamhuri;
2. Mlalamikiwa achapishe ufafanuzi wa habari iliyochapishwa baada ya kupata taarifa toka kwa upande wa Mlalamikaji.

### Maelezo ya Mlalamikiwa

Mlalamikiwa alitoa maelezo marefu kuonyesha jinsi yeye mwenyewe kama Naibu Mhariri Mtendaji alivyofanya jitihada za kumpata mmiliki wa METL, Gulam Abbas Dewji, ambaye alisema wana uhusiano mzuri.

Mlalamikiwa alisema pamoja na jitihada zote alizofanya kabla ya habari inayolalamikiwa kuchapishwa, hakupata ushirikiano toka kwa Gulam, ambaye alitoa majibu ya mkato na kusema kinu chenyewe kimeshachukuliwa na serikali.

Mlalamikiwa aliendelea kueleza kuwa hata baada ya kupata barua ya MCT ikimjulisha kuhusu malalamiko ya METL, alifanya juhudi kumpata Gulam, lakini Gulam hakupokea simu zake wala kujibu ujumbe aliomtumia.

Mlalamikaji alisema kutokana na maelezo hayo, anaona itakuwa si haki gazeti kuamriwa kuomba radhi, bali wako tayari kuchapisha ufafanuzi.

Katika maelezo ya nyongeza (rejoinder) ya Mlalamikaji, alisema kuwa haikuwa sahihi kwa gazeti kumtafuta Bw. Gulam baada ya kupokea barua toka MCT kwa maana malalamiko yalikuwa yamewasilishwa na Idara ya Sheria ya METL na sio Bw. Gulam. Wakili alisema kwamba Mhariri alipaswa kuwatafuta Idara ya Sheria ili kujadili jambo hilo.

### Uamuzi wa Kamati

Baada ya wahusika kutoa maelezo yake Mwenyekiti aliongoza mashauriano ambapo hatimaye alitangaza uamuzi uliofikiwa (na kukubaliwa na pande zote mbili) kama ifuatavyo:

1. Gazeti la Jamhuri lichapishe ufafanuzi wa taarifa inayolalamikiwa katika toleo lake la Machi 15, 2022;
2. Ufafanuzi ukubaliwe na pande mbili (METL na Jamhuri) kabla ya kuchapishwa;
3. Haitakuwa na manufaa kwa METL wala Jamhuri kwa gazeti kuchapisha maombi ya radhi.

Kamati pia ilitoa mwongozo wa jumla kama ifuatavyo:

4. Ni muhimu vyanzo vya habari (sources) kutoa ushirikiano kwa vyombo vya habari pale vinapofuatwa. Vyombo vya habari havilazimiki kuacha stori kwa kuwa tu chanzo kimoja cha habari kimekataa kutoa ushirikiano;
5. Kwa upande wa vyombo vya habari, vizingatie dhima yake ya kutoa habari za kweli na zilizokamilika kwa umma.

### Kuhitimisha Lalamiko

Mlalamikaji na Mlalamikiwa walikubaliana na maamuzi ya Kamati ya Maadili ya Baraza la Habari Tanzania na kuahidi kuyatekeleza. Walimshukuru Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati kwa usuluhishi huo. Mwenyekiti aliahirisha shauri hadi tarehe 15 Machi 2022, ambapo shauri litafungwa baada ya Jamhuri kuchapisha ufafanuzi. Hakutakuwa na kikao bali shauri litafungwa kwa taarifa kwa pande zote mbili.

**Jaji Robert V. Makaramba**
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Maadili,**
**Baraza laHabari Tanzania (MCT)**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bravo Wizara ya Elimu ushirikishaji wa wadau

**JANA** Wizara ya Elimu, Sayansi na Tekonolojia, imesema imekamilisha uundaji wa mfumo wa kusahihisha mitihani, ambao utaanza na ya walimu wa vyuo vya ualimu, lengo likiwa kuepuka udanganyifu.

Mfumo huo ambao ni wa kwanza Afrika, umegharimu zaidi ya Sh. milioni 550, umeundwa na Watanzania wenyewe, jambo lililowezesha kupunguza gharama. Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, anasema mfumo huo utasaidia kupunguza au kumaliza udanganyifu kwenye mitihani kwa kuwa anayesahihisha swali moja hatajua anasahihisha mtihani wa nani kwa kuwa hataona namba wala jina.

Alisema baada ya kusahihisha utakwenda kwa anayekagua, anayehakiki na baadaye kuwekewa alama, na kwamba wanaamini kwa utaratibu huo mfumo utadhibiti udanganyifu.

Alisema kwa sasa mfumo utafanyiwa marekebisho kwa kusahihisha mitihani ya walimu wa vyuo vya ualimu na baadaye utasambazwa maeneo mengine, ili kujiridhisha kama inafanyakazi kwa ufanisi unaotakiwa. Alisema lengo ni kuziba mianya yote na kuhakikisha wanaofaulu wanakuwa ni wale waliofanya vizuri inavyotakiwa, na siyo kwa sababu wamesahihishiwa ndivyo sivyo.

Kuvuja kwa mitihani au udanganyifu kwa kuwafaulisha wasiostahili ni hatari kwa taifa kwa kuwa linazalisha watu wasio na sifa zinazotakiwa kwa kuwa walishinda mitihani kwa mbinu chafu, ndiyo maana kumekuwa na jitihada nyingi za kudhibiti ili kutoharibu ubora wa mfumo wa elimu ya nchi.

Tunapongeza sana jitihada za Baraza la Mitihani la Taifa ( NECTA) kuunda mfumo huo zikiwa ni jitihada za kukdhibiti vitendo vya ovyo vya udanganyifu, ambavyo vimewachochea vijana wetu shuleni na vyuo vilivyoko chini ya NECTA kujiingiza katika mbinu chafu wa wizi wa mitihani badala ya kujiamini na kusoma kwa bidii.

Tunatarajia kuwa jitihada zaidi ikiwamo kubuni mifumo mingine ya kudhibiti udanganyifu katika mitihani unatakuwa endelevu, ili kuhakikisha wanapatikana wahitimu wanaokidhi viwango vya kitaifa na kimataifa. Bila hatua, tunaweza kujikuta tukizalisha taifa la wahitimu wajinga badala ya walioelimika na wenye viwango, hivyo kusababisha watu wetu kushindwa kushindana katika soko la ajira ndani na nje ya Tanzania.

Jitihada nyingine za wizara ni kufanya mabadiliko ya mitaala na sera za elimu nchini, ili kuhakikisha inaendana na mabadiliko ya dunia, kuacha utaratibu wa kukariri wanafunzi bali waweze kujiajiri watakapomaliza.

Waziri anakiri kuwa mfumo wa elimu uliopo sasa unamfanya mwanafunzi kukariri zaidi, anajifunza mambo mengi ambayo kimsingi hayamsaidii kwenye maisha yake, na ndiyo maana kumekuwa na wahitimu waliofaulu vizuri, lakini wanapofika kazini wanashindwa kufanya vizuri. Tunapongeza utaratibu wa sasa ambao utashirikisha wadau wote muhimu, ikiwamo sekta binafsi katika kujadili mitaala na sera, ili ipatikane nyaraka ambayo ni shirikishi kwa Watanzania wote.


Aidha, tunaridhishwa na uamuzi wa kuwa na rasimu ya kupeleka kwa wadau ambayo inaandaliwa na timu ya wataalamu, itawasilishwa kwenye kongamano la wadau litakalofanyika Mei mwaka huu.

Pia, tunapongeza msimamo wa waziri kuwa mabadiliko mbalimbali ya elimu hayatafanywa na wataalamu pekee kujifungia kwamba wanajua kila kitu, utakuwa shirikishi jambo ambalo lilikosekana kwenye mfumo wetu wa elimu na kuachwa kuwa maamuzi ya waziri na wataalamu wake na ndiyo maana tuliona kuna wakati michezo, masomo ya michepua ya kilimo na biashara yaliondolewa.

Mamlaka ya waziri kufanya mabadiliko ya mfumo wa elimu bila kushirikisha wadau kuiumiza na kuyumbisha sekta hiyo, hivyo ushirikishaji wa sasa unaleta matumaini.

Tunapozungumzia mitaala na mitihani ni jambo muhimu kwa mustakabali wa nchi, linahitaji umakini , ndiyo maana tunasema jitihada ziendelee kuhakikisha kinachopatikana ndicho kitaongoza elimu ya nchi hii kwa miaka mingi ijayo. Kwa muda mrefu kumekuwa na kiu ya kufumua mfumo wa elimu kwa kuwa haukidhi mahitaji ya sasa na utakapofumuliwa maana yake inatakiwa kupata nyaraka za kuongoza kwa miaka mingi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ujumbe wangu Siku ya Mwanamke, tumtafakari kwa kina yu nani kwetu

Na Yasmine Protace

**NI** juzi tu ilikuwa Maadhimisho ya Siku ya Mwanamke Duniani, kwa maana ya kilele siku ya Machi 8 ya kila mwaka, huwa kunafanyika maadhimisho hayo.

Hapo utakuta watu wanashika mabango yenye ujumbe wa namna mbalimbali, lakini kulia au kushoto, juu au chini zinaangukia ama kutetea au kusifu maslahi ya kinamama.

Ni aina ya ujumbe unaozungumzia mustakabali wa mwanamama katika mfumo na maisha yake endelevu wakati wote, katika dhana ya maendeleo endelevu.

Msingi uliko, kila ujumbe unaobebwa huwa una maana yake kubwa kwa kumtoa mwanamke sehemu moja kwenda sehemu nyingine, kutoka ngazi moja hadi nyingine.

Hivi karibuni washiriki wa semina za jinsia na maendeleo GDSD nchini, walijadili mada iliyokuwa ikisema

kuelekea Siku ya Wanawaake Duniani, maana yake imeshapita, iliangalia ni ulikosimama mtazamo wa jamii katika maendeleo endelevu ndani ya maslahi walio nayo.

Mshiriki wa mjumuiko huo wa GDSD, Jamal Juma, anasema kinachotakiwa sasa ni kutoa mfumo mzizi wa dume ambao bado upo katika maisha, ukionyesha hali ya mwanamke kutokubalika katika kushika madaraka katika baadhi ya familia.

Anasema mwanamke anapowezeshwa ana nafasi, hivyo cha muhimu kinachotakiwa ni kuwapo usawa wa kijinsia uwepo kati yake na mwanaume.

Pia ni mtazamo unaosonga kwamba hata utendaji wa jinsia, mwanamama ana uwezo wa kumiliki ardhi na hatua ilikofika ni kwamba, kinamama wanaaminiwa katika nafasi za utendaji.

Hawa Ally, anasema serikali inatakiwa iendane na kasi katika kumpatia maendeleo mwanamke, akitumia kauli

> **Msingi uliko, kila ujumbe unaobebwa huwa una maana yake kubwa kwa kumtoa mwanamke sehemu moja kwenda sehemu nyingine, kutoka ngazi moja hadi nyingine.**

"mwanamke akiwezeshwa ana uwezo mkubwa wa kuleta maendeleo katika eneo hilo."

Kuhusu maendeleo endelevu katika maeneo wanayoishi, Zuwena Shabani, anasema kuwapo kwa barabara zenye lami katika maeneo yao kumewasaidia, sasa biashara zimeongezeka, nyumba za kupanga nazo zimekuwa nyingi, hata kupangishwa watu wa aina mbalimbali, wakiwamo wasomi wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu.

"Kuwapo kwa uzuri wa barabara kumesaidia nyumba kuboreshwa kuongezeka kwa biashara katika maeneo hayo na hali hiyo kumfanya mkazi wa eneo hilo kuwa na maendeleo," anasema.

Robert James, mshiriki wa GDSD anasema, kuwapo maendeleo endelevu maana yake ni kwamba, hata vizazi vinatakiwa kufikia mkanufaika na maendeleo hayo.

Anasema rasilimali zinapaswa kusimamiwa vizuri, ili ziwe na nafasi ya kuwanufaisha watu na vizazi vyao katika mtazamo huo endelevu.

Maoni yangu ni kwamba, yanayojiri katika mandhari ya kijinsia na husUSAn kumwendeleza mwanamke, ina maana katika tafsiri pana na ya mwanadamu na jamii inavyoishi.

Huyu wa jinsia ya kike akiwezesha na hata akasimama imara ndani ya mfumo wake kijamii, iwe kiuchumi na hata kisiasa au mengineyo ndani ya mustakabali wetu wa kimaisha, ni wazi atakuwa anasonga mbele.

Kwa asili ya binadamu, mara zote anaishi ndani ya mjumuiko wa kijamii ambao unategemeana katika namna nyingi. Hapo kijinsia ni kwamba, kuanzia kimaumbile na asili, jinsia ya kile na kiume zinategemeana, hivyo inapoleta uhalali namna upande mmoja ukautegemea upande mwingine.

# Gwajima awapa tuzo wanawake wafanyabiashara

**Na Joseph Mwendapole**

WANAWAKE 35 wamepewa tuzo ya umahiri kwenye biashara zilizotolewa na Chama cha Wanawake Wafanyabiashara (TWCC).

Tuzo hizo walikabidhiwa jana na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wanawake, Watoto na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, kwenye hafla iliyofanyika ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Dk. Gwajima alisema wanawake wanaweza kufanya mambo makubwa kwenye jamii na kuwataka wanaume kuwapa nafasi ya kwenda kufanya biashara.

Dk. Gwajima aliipongeza TWCC kwa kuandaa tuzo hizo na aliwataka mwakani waongeze idadi ya tuzo hizo hata zifikie 150 ili kuendelea kuwapa moyo wanawake kuendelea kufanya vizuri kwenye biashara.

"Hizi ni tuzo muhimu sana kwa wanawake na nawashukuru wafadhili wa tuzo hizi na nawapa changamoto TWCC ongezeni idadi ya tuzo hizi hata zifikie 150 na hii itasaidia kuwapa moyo wanawake kwamba wanaweza kufanya mambo makubwa," alisema.

Alisema ni muhimu wanawake wakafanya biashara na kuinua kipato cha familia badala ya kumwachia mzigo baba peke yake kwa kuwa hali hiyo inaweza kumsababishia msongo wa mawazo na kusababisha apate maradhi au kifo cha mapema.

Waziri alisema kuna fursa nyingi za mikopo ya riba nafuu ambayo imekuwa ikitangazwa na serikali na taasisi nyingi za fedha hivyo ni wajibu wa wanawake kuzifuatilia na kuzichangamkia kila zinapotokea.

Mtendaji Mkuu wa TWCC, Mwajuma Hamza, alisema kulikuwa na majaji watano kutoka taasisi mbalimbali ambao walichuja majina ya wafanyabiashara hao kwenye sekta 16 zilizokuwa zikishindaniwa.

Alisema tuzo hizo zilitolewa baada ya maonyesho ya wiki moja ya wajasiriamali wanawake yaliyofanyika kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam na kufadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ).

Baadhi ya vigezo walivyoangalia, kwa mujibu wa Hamza, ni uendelevu wa biashara husika ili wasimpe mtu tuzo na biashara yake ikafa na waliangalia pia mikakati ya biashara husika.

Alisema kigezo kingine ni biashara iwe imerasimishwa na iwe na nembo ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) pamoja na umiliki wa biashara husika.

Mbali na GIZ, wafadhili wengine ni Trade Mark East Africa na benki za CRDB, NMB, NBC.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima (kushoto), akipokelewa na wanachama wa Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC), alipowasili kwenye ukumbi wa Mlimani City, mkoani Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kutoa tuzo kwa wanawake waliofanya vizuri kwenye sekta ya viwanda. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# RC: Msiwakimbie maofisa wa TRA

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amewataka wafanyabiashara mkoani hapa kutoa ushirikiano wa kutosha kwa maofisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA) watakaowatembelea katika maeneo yao ya biashara kutekeleza kampeni ya mlango kwa mlango.

Kampeni hiyo ina lengo la kutoa elimu ya kodi na kusikiliza kero za wafanyabiashara na kuzitatua.

Mtaka alisema juzi ofisini kwake kuwa wafanyabiashara wanapaswa kuondokana na hofu dhidi ya maofisa wa TRA wanaowatembelea katika maduka yao na kuwapa elimu ya kodi.

Alisema TRA kuwatembelea wafanyabiashara hao katika maduka yao ni fursa wanayopaswa kuitumia ipasavyo ili kupata elimu kuhusu kodi, umuhimu wake na taratibu sahihi za kuzingatia katika uendeshaji wa biashara.

"Wafanyabiashara walichukulie hili jambo katika mtazamo chanya, watoke kwenye hofu kwamba ukimwona ofisa wa TRA unakimbia. Rai yangu kwao waitumie hii fursa vizuri, waulize maswali na kutoa kero zao," alisema Mtaka.

Mwakilishi wa Meneja wa TRA Mkoa wa Dodoma, Philipo Eliamini, alisema baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa na kero kadhaa zinazowakabili katika biashara zao, hivyo kampeni ya TRA itakuwa na manufaa kwao.

Alisema uamuzi wa TRA kuwatembelea na kusikiliza kero zao na kuzitatua, utajenga uhusiano mzuri kati ya TRA na wafanyabiashara na kodi itakusanywa kwa hiari.

"Rai yetu tunawaomba wafanyabiashara wa Dodoma muwe huru kuuliza maswali, kutoa maoni na kutaja kero zenu ili tuweze kuzitatua na ili muwe walipakodi wazuri lakini mkumbuke kutoa risiti za elektroniki kila mnapofanya mauzo yenu," alisema Eliamini.

Mbunge na Balozi wa Kodi wa Hiari, Zulfa Omary Mmaka, alitoa rai yake kwa wafanyabiashara mkoani hapa kuitikia wito wa kutoa ushirikiano katika kampeni hiyo ya elimu kwa mlipakodi.

TRA inaendelea na kampeni yake hiyo ya utoaji elimu kwa mlipakodi ya mlango kwa mlango ikiwa na lengo la kuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiari na kukuza wigo wa walipakodi nchini. Kampeni hiyo kwa sasa inaendelea katika mikoa ya Dodoma na Manyara ilikoanza Machi 7 hadi 19 mwaka huu.

# DART yawakumbuka wagonjwa wa Tumbi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAKALA wa mabasi yaendayo haraka (DART) unatarajia kuanzisha safari za kuingia katika Hospitali ya Tumbi, Kibaha kurahisisha usafiri kwa wagonjwa.

Hayo yameelezwa na Mhandisi Philemon Mzee kwa niaba ya Mtendaji Mkuu wa DART katika Hospitali ya Tumbi walipofika kutoa misaada ya vifaa kwa wagonjwa ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Mzee alisema baada ya kufanikisha kufikisha mabasi Kibaha Mjini sasa wana nia ya kuanzisha safari kufika katika Hospitali ya Tumbi ili wagonjwa na wanaowasindikiza waondokane na adha ya usafiri.

Msaada uliyotolewa na DART kwa wagonjwa na uongozi wa hospitali hiyo ni mashuka, kiti cha kubebea wagonjwa, miswaki, sabuni na mafuta ya kupaka vyenye thamani ya Sh. milioni mbili.

Naye Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi kutoka UDART, Zaituni Hassan, alisema kwa sasa mabasi 19 yanaenda Kibaha kila baada ya dakika tano hadi sita, na lengo lao ni kufikisha huduma katika Hospitali ya Tumbi.

Alisema walianza kutoa misaada katika Hospitali ya Mloganzila na baadaye Tumbi Kibaha.

Daktari Kiongozi wa Hospitali ya Tumbi, Silas Msangi, aliishukuru DART kwa misaada wa vifaa waliyotoa ambayo itazidi kuboresha huduma.

Baadhi ya wagonjwa waliopata misaada hiyo waliishukuru DART kwa kuwakumbuka, huku wakiomba wadau wengine wanaoguswa kuwasaidia wagonjwa na vifaa kwenye hospitali hiyo.

# Vyuo vikuu vyapewa changamoto utafiti kutatua matatizo ya jamii

**Na Joseph Mwendapole**

VYUO vikuu nchini vimeshauriwa kusambaza utafiti vinaofanya kwa wahusika ili kuwasaidia kukabiliana na changamoto mbalimbali badala ya kuziweka kwenye makabati.

Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Dk. Albina Chuwa, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano kuhusu masuala ya takwimu ulioandaliwa na asasi ya Tanzania Data Lab.

Mkutano huo uliowashirikisha wanafunzi wa vyuo vikuu mbalimbali nchini, ulijadili umuhimu wa sayansi ya data katika afya ya wanawake na usalama na namna ya kuongeza ushiriki wa wasichana kwenye masomo ya sayansi.

Alisema uzoefu unaonyesha kuwa vyuo vikuu vingi vimekuwa vikifanya utafiti ambao hauwafikii walengwa, hivyo kutoleta tija yoyote kwa taifa licha ya rasilimali nyingi kuwa zimetumika katika kufanya utafiti.

"Vyuo vinafanya tafiti (utafiti) nzuri (mzuri) sana kwa mfano utafiti tuliosikia leo unahusu mwanamke na afya. Wameufanya vizuri sana kwa sababu wameangalia mwanamke anavyohusishwa kwenye masuala ya afya lakini utafiti kama huu uwafikie walenga ili uwe na manufaa," alisema Dk. Chuwa.

Alisema kuna haja kwa watoto wa kike kuhamasishwa kupenda masomo ya sayansi kwa kuwa uzoefu unaonyesha kuwa wengi hawayapendi na wamekuwa wakiona kama ya wanaume. Kwa mujibu wa Dk. Chuwa, asilimia 70 ya wanawake wanajihusisha na kilimo si kwa sababu wanapenda bali kutokana na kukosa elimu itakayowawezesha kufanya kazi za ofisini kama kukusanya data.

Aisema sehemu nyingi za kazi za ofisini wanaume wanachukua asilimia kubwa kutokana na kupata fursa ya kujiendeleza kwenye masomo mbalimbali yanayowawezesha kupata ujuzi tofauti na ilivyo kwa wanawake.

Dk. Chuwa alisema kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani suala la takwimu ni jambo muhimu kwa kuwa litatoa majibu ya kwa nini wamebaki nyuma kwenye mambo mengi ili hatua zichukulie kubadili hali hiyo.

Vile vile aliwataka wazazi watimize wajibu wao wa kuhamasisha watoto wa kike kusomea masomo ya sayansi na kuwaondolea fikra kwamba masomo hayo ni ya wanaume.

Alisema wazazi wana wajibu mkubwa kwenye malezi ya kuhakikisha watoto wanachukua mwelekeo sahihi wa maisha kwa sababu wakiachwa wataishia kuangalia mambo ya ovyo yaliyoko kwenye mitandao badala ya kujifunza mema.

Naye Mkurugenzi wa Mafunzo na Sayansi ya Data, kwenye asasi ya Tanzania Data Lab, Mahadia Tunga, alisema katika kuadhimisha siku ya wanawake duniani wameamua kuangazia mchango wa sayansi ya data katika kuimarisha afya ya wanawake na usalama.



Msomaji maarufu wa Quran Duniani kutoka nchini Marekani, Dk. Hassan Saleh, akijiandaa kupanda mti wa mwembe katika eneo la Wilaya ya Kigamboni, mkoani Dar es Salaam mapema wiki hii, akiunga mkono juhudi za serikali katika uhifadhi wa mazingira nchini. Kulia kwake ni Mkurugenzi wa Taasisi za Jumuiya ya Kuhifadhi Quran Tukufu Tanzania, Shehe Othuman Kaporo, Mkurugenzi wa Property International Ltd, Abdulhalim Zahran na viongozi wengine wakiwa katika kampeni maalum Quran na Mazingira yenye lengo la kupanda miti 2000 na uzinduzi wa miaka 30 ya Tuzo za Kimataifa za Quran 2022. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbunge wa Hai atangaza kumaliza chuki na Mbowe

**Na Godfrey Mushi, HAI**

MBUNGE wa Hai mkoani Kilimanjaro, Saashisha Mafuwe (CCM), amesema yeye si muumini wa siasa za uadui, chuki na kuumizana, ndio maana alidiriki kumkaribisha nyumbani, Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe.

Mafuwe alitoa kauli hiyo jana, alipokuwa akizungumza na wakazi wa Kata ya Narumu katika mfululizo wa ziara zake jimboni humo.

Machi 4, mwaka huu, Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP), aliwasilisha mahakamani hati ya kutokuwa na nia ya kuendelea na kesi iliyokuwa ikimkabili Mbowe na wenzake watatu katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi.

Akizungumza na wananchi wa Narumu, Mbunge huyo alisema: "Acheni kuumizana kwa sababu ya siasa, acheni kuchukiana kwa ajili ya siasa, mmeona kilichotokea, baada ya Freeman Mbowe kuachiwa aliendа wapi. Alienda kwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa.

"Na mimi alivyotoka (Mbowe), si niliandika nikamwambia karibu nyumbani kaka; huo ndio undugu, hatutaki siasa za uadui za kuumizana.

"Halafu Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, anaenda kwa Mwenyekiti wa CCM Taifa wanazungumza, mbunge anaenda kwa aliyekuwa mbunge, simnasikia misiba yote ya kwa Mbowe naendaga? Kukiwa na sherehe mimi niko naye, halafu wewe unayegombana unagombana nini mzee! Utabaki peke yako, nakwambia mzee tafuta hela (pesa), utabaki peke yako."

Aliongeza: "Sisi tunaelewana tukimaliza kampeni tunakaa wote tunakunywa soda, tunakunywa kahawa yetu. Nyie kununiana, acheni hiyo biashara. Siasa nzuri ndio hii tunayofanya ya maji, umeme, kilimo, hiyo ndiyo siasa, sio maneno na ugomvi ugomvi.

"Mnakuja kuumizana wenyewe kwa wenyewe hapa, halafu sisi baadaye tunaelewana, tunawaacha na majeraha. Tuache hayo mambo, watu wa Narumu nawapenda sana, nawaombeni tufanye siasa za kistaarabu na siasa zilishaisha sasa ni muda wa kazi."

Aidha, Mbunge huyo aliisema, "Lakini kuna kitu mmejifunza, si ndio hiki mmejifunza hapa, wale ambao mlikuwa mnapambana, sisi tumeshaelewana huko, mtajua wenyewe. Cha kuambiwa changanya na cha kwako, pambana na tumbo lako, pambana na nyumba yako, tukija tukiwaeleza maneno tupeni tukafanye kazi."

"Mmenituma mmeona kazi ninayoifanya, na sasa hivi naanza vijiji mpaka nitoboe vitongoji vyote viingine kwenye Hansad (kumbukumbu rasmi) za Bunge. Keshokutwa mtasikia tela, ntataja vyote hicho ndicho mlichonituma na ndio siasa hiyo.

Nadhani mmeona na ninyi Mbunge wenu siingii kwenye maugomvi ya watu au mmeshasikia nazungumza mambo ya kitaifa, naongea mlichonituma mimi, maji, barabara, umeme.

"Sasa na ninyi si muige, kwa nini mlete mambo ya chuki chuki. Kwa nini mnaumizana wenyewe kwa wenyewe. Halafu mnaumizana ili wewe uwe nani? Akionya kuhusu vitendo hivyo, Mafuwe alisema kama mbunge hana chuki na mtu, Mwenyekiti wa Taifa, hana chuki na mtu, wewe hiyo chuki unaitoa wapi? Ndugu zanguni niwaombe tupendane, tushirikiane."

## Shule yapata msaada madawati 30

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

SHULE ya Msingi Lubaga Manispaa ya Shinyanga, imepewa msaada wa madawati 30 na kikundi cha wanawake Manispaa ya Shinyanga (Women for Change).

Shule hiyo inakabiliwa na upungufu wa madawati 73 na baada ya kupokea msaada huo imesaliwa na upungufu wa madawati 43.

Mwenyekiti wa kikundi hicho, Ansila Benedict, alisema kuwa kila mwaka wamekuwa wakiadhimisha sherehe yao ya wanawake (Women's day Out), na kabla ya kufanyika kwa sherehe hiyo wana utaratibu wa kutoa misaada mbalimbali kwa jamii.

Alisema kwa mwaka huu wametoa madawati katika Shule ya Msingi Lubaga, Manispaa ya Shinyanga ili kupunguza tatizo la upungufu mkubwa wa madawati shuleni hapo.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, amekipongeza kikundi hicho cha wanawake 'Women for Change', kwa kushirikiana na serikali kutatua changamoto za elimu, huku akiwaunga mkono kutoa zawadi ya kiti na meza kwa ajili ya matumizi ya mwalimu mkuu wa shule hiyo.

Aidha, alisema mkakati wa serikali kwa shule zote za Manispaa ya Shinyanga na Halmashauri ya wilayani Shinyanga, ni kuhakikisha hakuna mwanafunzi atakayesoma akiwa hana dawati, kiti wala meza na zoezi hilo kwa shule za sekondari wamemaliza na sasa wanaelekeza nguvu kwa shule za msingi.

Pia, amewapongeza walimu wa shule hiyo ya Lubaga kwa kujituma kufundisha wanafunzi na kushika nafasi ya kwanza kwenye matokeo ya darasa la saba kwa shule za Serikali Manispaa ya Shinyanga na kuwasihi waendelee na kasi hiyo hiyo, huku akiwataka wasome kwa bidii ili watimize ndoto zao na kuja kuwa viongozi wa taifa hapo baadaye.

Alisema kwa changamoto ambayo bado inaikabili shule hiyo ikiwamo upungufu wa viti na meza kwa walimu, ameahidi kuwa atalitatua huku akiwataka na walimu katika shule nyingine za serikali wajitahidi kufundisha wanafunzi na watakaofanya vizuri watapewa zawadi.

Katika hatua nyingine Mboneko alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa Sh. milioni 600 kwa ajili ya kujenga shule mpya ya Sekondari Lubaga, na wameshapokea Sh. milioni 470 na ujenzi unaendelea.

Naye Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo Stella Halimoja, amekishukuru kikundi hicho kwa kuwapatia msaada huo utakaopunguza upungufu uliopo wa madawati shuleni hapo, huku akimshukuru pia Mkuu wa wilaya kwa kumpatia zawadi ya kiti na meza.

Baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo kwa nyakati tofauti, walisema wanapokuwa wakisoma kwa kubanana kutokana na upungufu wa madawati wamekuwa wakishindwa kuandika vizuri na kukabiliwa na miandiko mibaya na hawasomi kwa raha na kushukuru msaada huo wa madawati 30.

# Watoto wenye ulemavu kuwezeshwa kwa elimu

Na Frank Monyo

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, amesema serikali itaendelea kuboresha miundombinu katika Chuo cha Ufundi cha Wenye Ulemavu Yombo Kiwalani mkoani Dar es Salaam ili kila mtoto mwenye ulemavu aweze kupata elimu ya ufundi stadi.

Kauli hiyo aliitoa juzi wakati akipokea msaada wa magodoro 80 na vitanda 40 uliotolewa na Mfuko wa Self wenye thamani ya Sh. milioni 29.

Msaada huo ulitolewa wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ili kupunguza adha ya uhaba wa vifaa vya malazi kwa wanafunzi wa chuo hicho.

Katambi alisema, taasisi hiyo imefanya jambo jema kwa kusaidia chuo hicho kikongwe cha wenye ulemavu nchini kupata vifaa hivyo kwa ajili ya malazi ya wanafunzi, huku akisisitiza kuwa serikali itaendelea kuboresha sera na kubadilisha sheria ili kuhakikisha haki za wenye ulemavu nchini zinalindwa kikamilifu.

"Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imetenga Sh. bilioni 8 ili kuboresha vyuo vyote vya watu wenye ulemavu nchini. Msaada huu uliotolewa unaunga mkono jitihada za serikali katika kupunguza adha ya vifaa vya malazi kwa wanafunzi wa chuo hicho," alisema Katambi.

Aliongeza kuwa vyuo vya ufundi vya watu wenye ulemavu vipo sita nchini ambavyo vipo Tanga, Tabora, Dar es Salaam, Mtwara, Mwanza na Zanzibar.

"Tunajua kwamba watu wenye ulemavu wapo katika makundi maalum na wanahitaji kupata mafunzo ya ufundi stadi kulingana na makundi yao. Serikali iliamua kuanzisha vyuo hivyo ili kila Mtanzania ashiriki katika shughuli za kijamii na kiuchumi za kujenga taifa," alisema.

Katambi aliwashukuru watendaji wa mfuko huo kwa kusaidia vitanda na magodoro wanafunzi hao na kuzitaka taasisi na kampuni mbalimbali kuiga mfano huo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Self, Mudith Cheyo, alisema mfuko huo ulianzishwa Septemba 2014 kwa lengo la kutekeleza sera ya uwezeshaji wananchi kiuchumi.

"Leo tumekuja kutoa msaada kwa chuo hiki cha watu wenye ulemavu ili kuunga mkono serikali katika kusaidia watu wenye ulemavu, hiyo itasaidia kupunguza adha ya uhaba wa vifaa vya malazi na pia wajisikie tunawapenda," alisema Cheyo.

Aliongeza kuwa mfuko huo unatoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wananchi wenye kipato cha chini hususani vijijini na kwamba hadi kufikia Desemba 2021 wametoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 257 kwa wakopaji, 187,731 pamoja na kuendelea kutoa mikopo kwenye taasisi mbalimbali.

Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Mariam Chillangwa, alisema chuo kinatoa mafunzo ya ufundi stadi kama vile umeme wa majumbani, useremala, ushonaji, utengenezaji wa makabati na upishi.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Doroth Gwajima (wapili kushoto), akipata maelezo kuhusu mfumo unaotoa mafunzo kwa wafanyakazi wa afya kwa njia ya simu ya mkononi unaoitwa LEAP unavyofanya kazi, kutoka kwa Ofisa Teknolojia ya Mawasiliano wa Shirika la Amref Health Africa, Ezra Mfaume (aliyesimama kulia), alipotembelea maonyesho yaliyoandaliwa na Muungano wa Asasi za Kiraia (Mkuki coalition), kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mtaa Dar waanzisha kampeni uhamasishaji chanjo UVIKO-19

Na Sabato Kasika

VIONGOZI wa serikali ya mtaa wa Mwananyamala Kisiwani mkoani Dar es Salaam, wameanzisha kampeni ya kuhamasisha chanjo ya UVIKO-19 kwa wakazi wa mtaa huo, kupitia mikutano ya hadhara.

Mwenyekiti wa serikali ya mtaa huo, Ismail Rashid aliliambia gazeti hili jana kuwa kila wanapoitisha mikutano ya kujadili maendeleo ya mtaa wao, ajenda ya kwanza ni kuhimiza chanjo.

Alisema, kipindi hiki ambacho kumekuwapo na matukio mengi katika jamii, yakiwamo ya ukatili wa kijinsia, wanalazimika kuitisha mikutano ya mara kwa mara ambayo wanaitumia kuhakikisha wananchi wanapata elimu ya chanjo.

"Hatua hiyo imesaidia kubadilisha mtazamo wa watu wengi ambao awali walikuwa hawataki kuchanja na kutegemea sana kupiga nyungu wakihofia usalama wa chanjo, sasa wamebadilika wanachanjwa," alisema Rashid.

Alisema, hatua ya kuifanya ajenda ya chanjo kuwa ya kwanza kwenye mikutano yao kabla ya kuendelea na nyingine, imepanua uelewa wa wakazi wa mtaa wake na kwamba mwitikio wa chanjo unaendelea kuongezeka.

"Kwanza kabisa ni kwamba mimi na wajumbe wangu watano na mtendaji wa mtaa tumeshachanja, hivyo tunahimiza wananchi tukiwa na uhakika wa ubora wa chanjo ya kujikinga na UVIKO-19," alisema.

Alifafanua kuwa kwa wale ambao wanakuwa tayari kuchanjwa, huwa wanaelekezwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mwanyamala kupata huduma hiyo, kwa kuwa mtaa wake hauna kituo cha kutolea chanjo.

"Wale wanaotaka kusindikizwa, huwa tunawapeleka, na ninaamini kwamba kasi ya wanaochanjwa inaweza kuongezeka hasa baada ya kuwapo kwa takwimu kuwa Dar es Salaam, inaongoza kwa maambukizi," alisema.

Alisema, amesikia takwimu za Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe, kuhusu mwenendo wa ugonjwa wa UVIKO-19 nchini, ikionyesha kuwa watu 33,726 wamethibitika kukumbwa nao, huku 800 wakipoteza maisha kwa kipindi cha Machi, mwaka jana hadi Machi 4, mwaka huu.

Mwenyekiti huyo alisema, idadi hiyo ni kati ya 471,965 sawa na asilimia 7.1 na kwamba waliopoteza maisha ni asilimia 2.5 akionyesha kuwa kuanzia Februari 5 hadi Machi 4, mwaka huu, kulikuwa na walioripotiwa kupata ugonjwa huo kati ya watu 31,090 waliopimwa na vifo vinane katika mikoa ya Mwanza (vitano), Dodoma (viwili) na Kagera (kimoja).

"Lakini alifafanua kuwa katika wagonjwa hao, visa 290 vilivyothibitika, mkoa wa Dar es Salaam unaongoza kwa kuwa na wagonjwa 175. Takwimu hizo zinatosha kutuweka mguu sawa kwenye suala la kuhimiza chanjo," alisema.

Alisema, matamanio yake ni wananchi wa mtaa wa Mwananyamala Kisiwani kuachana na dhana potofu kuhusu chanjo na pia kufuata ushauri wa wataalamu wa afya na siyo kupiga nyungu.

## Wanawake SBL waonyesha uwezo wao kuendesha kiwanda

Na Mwandishi Wetu

TIMU ya vijana wa kike 13, wameonyesha kuwa wanawake wanaweza baada ya kupewa jukumu la kuendesha kiwanda cha kutengeneza pombe kali kinachomilikiwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) na kuifanya kwa ufanisi mkubwa.

Kiwanda hicho kinachotengeneza pombe kali aina ya Bongo Don, kipo Moshi mkoani Kilimanjaro na kinaendeshwa na wanawake tu.

Mmoja wa wafanyakazi wa kiwanda hicho, Evelyn John, aliliambia gazeti hili kuwa yeye pamoja na vijana wenzake wa kile wamekuwa wakikiendesha kiwanda hicho kwa ufanisi na kwamba anajisikia furaha kuwa sehemu ya timu hiyo.

"Ni jambo la kujivunia sisi kama vijana wa kike kuendesha kiwanda cha kisasa kama hiki kwa ufanisi mkubwa. Pamoja na kufanya kazi pia tumefundishwa namna ya kuwa imara, kukabiliana na changamoto na hivyo kuwa viongozi bora," alisema.

Aliishukuru Kampuni ya SBL kwa kutoa fursa kwa wanawake kuonyesha uwezo na kusisitiza kuwa wanawake wakipewa fursa wanaweza.

Betrida Cayus, fundi mitambo kiwandani hapo, anasema timu ya vijana wa kike inayoendesha kiwanda hicho imeweza kuonyesha uwezo ambao umewashangaza watu wengi wanaofika kuwatembelea.

"Kwa hiki tunachokifanya tunaondoa mtizamo kuwa kuna kazi ambazo wanawake hawawezi kuzifanya bila msaada wa wanaume. Ufanisi wetu kama timu na mtu mmoja mmoja ni ushahidi unaoongea juu ya uwezo wetu," alisema.

SBL imekuwa ni mdau mkubwa katika kuhamasisha usawa na ujumuifu kwa vitendo na imekuwa ikitekeleza programu mbalimbali za kusaidia wanawake.

Moja kati ya programu hizo ni ya ufadhili wa masomo ya kilimo inayojulikana kama Kilimo Viwanda ambayo imefadhili wanafunzi 200 mpaka hivi sasa ambao nusu yao ni watoto wa kike.

SBL pia inaendesha programu ya STEM ambayo huwachukua kutoka vyuoni vijana wa kike wanaofanya vizuri katika fani za sayansi, teknolojia pamoja na hisabati na kuwapa fursa ya kujifunza kwa vitendo kwa muda wa mwaka mmoja katika viwanda vyake.

# Kiini ongezeko saratani Kanda ya Ziwa chatajwa

**Na Richard Makore,** MWANZA

WATAALAMU wa Sekta ya Madini nchini wamesema kemikali aina ya zebaki inayotumika kuoshea mchanga wa dhahabu inasababisha wakazi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa kupata maradhi ya saratani.

Madhara mengine yaliyotajwa na wataalamu hao kuchangiwa na kemikali hiyo ni pamoja na kuzaliwa watoto wenye vichwa vikubwa na upofu.

Kutokana na baa hilo, wataalamu hao wameiomba serikali kukomesha matumizi ya zebaki ili kuokoa maisha ya wananchi.

Akizungumza katika kongamano la masuala ya madini lililofanyika jijini Mwanza jana, mtafiti katika sekta hiyo, Dk. Peter Kafumu, alisema matumizi ya kemikali aina ya zebaki yamepigwa marufuku na nchi mbalimbali duniani kutokana na kusababisha madhara ya kiafya.

Hata hivyo, Kafumu ambaye amewahi kuwa Kamishna wa Madini nchini kwa miaka sita, alisema mikoa ya Kanda ya Ziwa ina madini mengi na kwamba wachimbaji wanaotumia zebaki kuchenjua dhahabu ni hatari kiafya.

Kutokana na kuwapo tatizo hilo, Dk. Kafumu aliishauri serikali na wadau wengine kuendelea kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo ili kuachana na matumizi ya kemikali hizo.

"Wananchi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa wanaoongoza kwa ugonjwa wa kansa na hili ni tatizo kubwa. Kuna haja serikali kuchukua hatua za makusudi ili kukomesha hali hiyo," alishauri.

Dk. Kafumu ambaye ni mtafiti mbobezi katika Sekta ya Madini, alisema wataalamu kadhaa wamefanya utafiti na kubaini kuwapo athari hizo za kiafya kutokana na matumizi ya zebaki.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Ulinzi wa Maliasili, ambaye anafanya utafiti kwenye Sekta ya Madini, Silas Olan'g, alisema kemikali hizo zimepigwa marufuku, lakini zinaingia nchini kwa njia za panya. Alisema nchi nyingi duniani zimepiga marufuku kemikali hizo na kuomba serikali kuongeza udhibiti ili zisiingie nchini.

Olan'g alisema wamebaini kemikali hizo kuleta madhara ya kiafya ikiwamo ugonjwa wa saratani kwa kuwa zinamwagika kwenye maji wakati wa kuosha mchanga wa dhahabu na kisha wananchi kuyatumia maji hayo kwa kuyanywa na kuyaoga.

Akizungumzia tatizo hilo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Utafiti na Uchambuzi wa Sera (PADO) katika Sekta ya Madini, Profesa Sufian Bukukura, alisema licha ya madini kunufaisha taifa, kuna madhara yatokanayo na matumizi ya kemikali, hasa zebaki wakati wa uchenjuaji. Alisema wachimbaji wadogo wanahitaji elimu ili kuondokana na matumizi ya kemikali hizo pamoja na kukata magogo ya miti na kuyatumia kwenye mashimo wanayochimba dhahabu.

Ofisa huyo alisema ukataji wa miti unaleta madhara katika mazingira na kwamba wachimbaji wanalazimika kukata miti kutokana na kukosa elimu.

Aliomba serikali kuendelea kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo na kuwawezesha kupata teknolojia ya kisasa ili waweze kuchimba dhahabu kisasa pamoja na kuondokana na matumizi ya zebaki.




Mkuu wa Kitengo cha Mikopo ya magari cha Benki ya Stanbic Tanzania, John Mosha (watano kushoto) na Li Zhongyuan wa kampuni ya Sino Truck, wakiwa wameshika mfano wa ufunguo kuashiria makabidhiano ya malori 70 kwa Meneja Mkuu wa Kampuni ya Galco, Sultan Abdallah (kulia), jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Benki hiyo, kupitia huduma yao ya VAF ilikuwa na mchango mkubwa kufanikisha ununuzi wa malori hayo. Wengine ni wafanyakazi wa benki hiyo na GSM. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uuzaji nyama nje ulivyopaa kwa miezi 7

**Na Moshi Lusonzo**

BIASHARA ya uuzaji nyama nje ya nchi imekua kwa kasi hadi kufikia tani 5,340 katika kipindi cha nusu mwaka, kutoka tani 1,774.29 za mwaka jana.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alibainisha hayo wakati akitoa tathmini ya wizara yake ya mwaka mmoja tangu Rais Samia Suluhu Hassan, aingie madarakani.

Alisema mauzo ni kuanzia Julai, 2021 mpaka Januari mwaka huu, serikali imeingiza dola milioni 22.4 sawa na shilingi bilioni 52.1 kutoka 9.9 za mwaka uliopita.

Waziri Ndaki, alisema mafanikio hayo yanatokana na juhudi kubwa zilizofanywa na serikali kuimarisha sekta ya mifugo ikiwa ni pamoja na kuongeza mifumo ya udhibiti magonjwa na uhamasishaji wa ufugaji wa kisasa.

Alisema kutokana na kazi kubwa ya Rais Samia Suluhu Hassan, Tanzania imefanikiwa kupata soko la nyama katika nchi za Oman, Kuwait, Qatar, Saudi Arabia na Hong Kong.

Alisema soko la Saudi Arabia pekee wanahitaji tani 700,000 kwa mwaka na tayari wataalamu kutoka nchi hiyo wamekuja nchini kukagua baadhi ya viwanda vya kuchinja na kuchakata nyama na wameridhika.

Alisema katika mauzo hayo ya nje, uzalishaji wa ngozi ulizidi kuimarika kupitia sekta binafsi na kuwezesha uzalishaji wa viatu vya ngozi jozi 3,004,700, huku jumla ya vipande vya ngozi 73,607 vyenye thamani ya shilingi 460,043,750 viliuzwa nje ya nchi.

"Biashara ya ngozi imekuwa kwa kiwango kikubwa, sambamba na uzalishaji wa maziwa uliongezeka kwa asilimia 3.1 kutoka lita bilioni 12.1 hadi 3.1," alisema Waziri Ndaki.

Alisema sekta binafsi imechangia upatikanaji wa maziwa kutokana na kuwezesha uwepo wa vituo 238 vya kukusanyia na kupooza maziwa, huku viwanda vya kusindika mpaka sasa vipo 104.

Alieleza serikali inaendelea kufanya utambuzi wa mifugo kwa mfumo wa kielektroniki na mpaka kufikia Januari mwaka huu, jumla ya mifugo 1,504,659 katika mikoa 14 wametambuliwa ikiwamo ng'ombe 1,219,481, mbuzi 167,298, kondoo 61,571 na punda 56,309.

Upande wa Sekta ya Uvuvi, Waziri Ndaki, alisema serikali ya awamu ya sita imejizatiti kuwa kinara katika Afrika Mashariki kwa uzalishaji wa samaki kwa kuongeza uzalishaji wa bidhaa hiyo.

Alisema tayari wametangaza tenda ya ujenzi wa bandari kubwa ya samaki eneo la Kilwa na Sh. bilioni 50 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

" Sasa samaki wanachangia uhakika wa upatikanaji wa chakula na lishe kwa asilimia 30, na kuongeza ajira ya uvuvi kufikia 195,435 na wafanyabiashara wa samaki 4.5.

"Ongezeko hilo linatokana na serikali ya awamu ya sita kutekeleza mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish) ambao unalenga kuongeza faida za kiuchumi, kijamii na kimazingira ili kuwezesha uvuvi endelevu katika mwambao na ukanda wa uchumi wa Bahari," aliongeza.

## Wanaume washauriwa wasife na 'tai shingoni'

**Na Richard Makore,** MWANZA

SIKU ya Mwanamke Duniani iliyofanyika juzi katika mikoa mbalimbali hapa nchini, jijini Mwanza ilifanyika kwa staili na matamko tofauti, huku wanaume wakishauriwa kutokufa na 'tai shingoni' badala yake wajitokeze na kupaza sauti zao dhidi ya vitendo vya kikatili wanavyofanyiwa na wake zao.

Siku hiyo muhimu kwa wanawake, jana ilifanyika kimkoa katika viwanja vya Nyamagana, huku baadhi ya wadau wakipigwa butwaa baada ya kusikia kauli ya kuwataka wanaume wajitokeze ili kuelezea ukatili wanaofanyiwa majumbani.

Katika maadhimisho hayo ambayo yalihudhuriwa pia na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii na UKIMWI, yalitanguliwa na maonyesho ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na wanawake mkoani hapa.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilo la kiserikali ambalo linatetea haki za wanawake na watoto la Kivulini, Yassin Ally, alishauri wanaume kupaza sauti dhidi ya vitendo vya kikatili wanavyofanyiwa na wake zao.

Alisema licha ya kuwa idadi kubwa ya vitendo vya kikatili wanafanyiwa wanawake na watoto, lakini kundi la wanaume nalo linakutana na majanga hayo.

"Wanaume msikubali kufa na "tai shingoni' jitokezeni mpaze sauti zenu, mseme vitendo mnavyofanyiwa na wenza wenu, unakuta nyumbani wanaume hawaongei na wake zao, ukiuliza kitu hujibiwi, ukimwambia mwanamke geuka huku unakula kipepsi yote haya ni manyanyaso mjitokeze mseme," alisema Ally.

Alisema ili kutekeleza kauli inayosema kizazi cha haki na usawa ni lazima wanaume kujitokeza na kusema mabaya wanayokutana nayo katika familia zao hususani kutoka kwa wake zao.

Ally ambaye shirika lake limekuwa mstari wa mbele kutetea haki za wanyonge wakiwamo, wanawake, watoto, wenye ulemavu na wajane, alisema wanaume wengi hawasemi wala hawatangazi ukatili wanaokutana nao nyumbani.

"Mwanaume ukiulizwa vipi bwana, unasema 'no sweat' yani hakuna shida, wakati unakumbana na vitendo vibaya vya ukatili," alisema.

Kwa upande mwingine, Ally aliiomba jamii kuliona jukumu la kulea watoto ni la kwao badala ya kumwachia mzazi peke yake kufanya kazi hiyo.

Alisema mzazi hawezi kulea mtoto peke yake na kwamba masuala ya kulea watoto yakirudishwa kwa jamii, kunaweza kupunguza vitendo vya kikatili vinavyofanyika katika sehemu mbalimbali nchini.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, aliwataka wanawake kuendelea kusimama imara na kupigania haki zao za msingi.

Makilagi ambaye maadhimisho hayo yalifanyika wilayani kwake, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyopigania haki za wanawake na kuhakikisha vitendo vya ukatili dhidi yao vinakomeshwa.

Maadhimisho hayo ya Siku ya Mwanamke Duniani, yalihudhuriwa na wanawake kutoka taasisi za umma, binafsi, wanafunzi, makundi maalum, wabunge pamoja na viongozi wa serikali.



Ukurasa 12

KILIMO CHA MWANI TANZANIA BARA ... Zao jipya linaloshikiliwa na kinamama, shamba lake ndani bahari mikoa Kusini




**Jiji Dodoma kuzaliwa upya kupitia ujenzi barabara Km. 112, kuungana kona zote**

Ukurasa 14

# BUFE

IJUMAA MACHI 11, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Bandari ya Tanga yasukwa upya kukidhi mahitaji soko sasa, yajayo

## • Ifikapo Oktoba; kuna gati jipya, kina chaongezwa

**Na Boniface Gideon, TANGA**

TANGA ni kati ya bandari tatu kuu nchini na za kihistoria. Nyinginezo ni Mtwara, pia Dar es Salaam ambayo ni kubwa na maarufu.

Pamoja na umaarufu na ukongwe wake, bandari ya Tanga imekuwa na upungufu katika eneo mojawapo, kwamba haina kina kirefu gatini, hata kuifanya ikapakua mzigo kwa msaada wa matishali, meli zikiegeshwa mbali zaidi.

Hiyo kwa muda mrefu imebaki kuwa kasoro dhidi ya wasifu ilio nao, kwani imechangia sana kuongezeka gharama za upakuaji na upakiaji mizigo kwa wafanyabiashara na wateja wengineo wanaotumia huduma ya bandari.

Ni walakini ambao sasa mamlaka ya kiserikali imeamua kuingilia kati kuitatua kwa kuchimba kina kirefu, sambamba na kuongezeka magati ya kupakua na kupakia mizigo, inayozaa tafsiri kwamba itasaidia kuongezeka idadi ya meli na wateja wanaoitumia.

Kwa ujumla inaelezwa, ni manufaa ambayo mageuzi na ufanisi wa maboresho hayo yanawagusa moja kwa moja watumiaji bandari, kuanzia wenyeji na watokao mikoa jirani kama vile Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

Hali kadhalika, inawagusa wateja wa kigeni waliolazimka hata kufuata huduma hiyo katika nchi jirani, hasa kwa watokao nchi za karibu kama Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).



Kazi ya ujenzi wa gati la Bandari ya Tanga, ikiendelea. **PICHA: BONIFACE GIDEON.**

Baadhi ya mizigo ya nchi hizo inategemea kupitishiwa bandarini hapo Tanga.Pia, sasa kuna manufaa mapya ya sasa yanajengwa kupitia bomba la mafuta ghafi linaloanzia Hoima nchini Uganda hadi Tanga Chongoleani yote yanatajwa kuongeza uchumi na ajira nyingi kwa vijana.

**ZIARA YA UKAGUZI**

Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), limefanya ziara bandarini Tanga kukagua ufanisi uliopo na mwenyekiti wake, Mussa Mandia, anasema ni aina ya ukaguzi wenye tafsiri pana, hata kugusa bandari ndogo na zilizopewa hadhi 'bubu.'

Kwa ujumla, Mandia anakiri kiridhishwa na kazi ya Upanuzi unaoendelea bandarini, akifafanua: "Tumekuja kutembelea Bandari za Tanga na siyo ya Tanga, kwa kuwa kuna bandari kubwa na bandari ndogo ndogo ambazo ni bubu.

"Tuliwahi kutoa maelekezo TPA (Mamlaka ya Bandari Tanzania) wazirasimishe bandari (bubu), ili kupunguza bandari bubu kwa manufaa ya taifa. Tumeona kwamba kazi inaendelea ya kuboresha Bandari ya Tanga.

"Kwa ajili ya kuimarisha operesheni za bandari kwa maana ya kubeba mizigo mingi na kwa njia ambayo ni salama zaidi, hilo ndilo jambo tunalosimamia pamoja na utendaji wa bandari" anaeleza Mandia

Pia, anakiri ameona kina cha bandari kinaongezwa kufikia mita 13, jambo litaloiwezesha meli kufika mpaka bandarini

Anasema, kinachofanyika sasa ni kuongeza kina cha bandari kutoka mita tatu hadi 13, jambo litaloziwezesha meli kuingia bandarini, tofauti na zamani operesheni ilifanyika katikati ya maji.

Mandia anaeleza matarajio ni baada ya ujenzi huo kukamilika mwezi Oktoba mwaka huu, meli kubwa zitatia nanga kwenye gati jpya, matarajio ni kwamba italeta tija katika upana wake, ikijumuisha usalama wa watu na mizigo inayopakuliwa na kupakiwa, huku pia ikiongezeka.

**WASIMAMIZI BANDARI**

Meneja wa Bandari ya Tanga, Masudi Mrisha, anasema ujenzi wa gati hizo utakapokamilika, utaleta ufanisi kwa shughuli zao bandarini, akifafanua:

"Ujenzi wa Gati mbili zenye urefu wa mita 450 unaenda kwa Kasi kubwa na ifikapo mwezi Mei, mita 150 za ujenzi wake utakua umekamilika na meli zenye urefu huo zitaweza kuingia bandarini na mpaka mwezi Oktoba, mita zote 450 zitakuwa zimekamilika."

Meneja huyo anaeleza kuwa ana matarajio baada ya kukamilika upanuzi, meli za aina mbalimbali zitaweza kuwasili bandarini hapo na kupakua mizigo kufikia tani zaidi ya milioni tatu kwa mwaka.

"Magari yataweza kuwasili na kushusha mizigo hapa, mizigo itaongezeka na shehena zitakazokuwa zinawasili zitapakuliwa kwa haraka," anasema Mrisha na kuongeza:

"Kwa sasa bandari inahudumia tani 71 8,400. Kukamilika kwa gati hizo mbili, bandari itaweza kuhudumia mzigo wa tani milioni tatu," anasema Meneja wa Bandari.

**WANA TANGA WANENA**

Abdalah Saleh, ni mkazi anayepata mkate wa kila siku katika shughuli za ujenzi huo, ana maoni kadhaa alipohojiwa na Nipashe, kwamba: "...ujenzi huu tumejipatia kazi, mwanzo tulikaa tu maskani tukiwa hatuna kazi, lakini leo hii tunashukuru mkono unaenda kinywani miezi zaidi ya minne."

Mwanamkasi Mwandorwa, anayeuza vyakula na vinywaji eneo la Bandari, naye ana neno lake kuwa: "Wametuletea Neema kubwa hasa kwa sisi kina mama ambao tunajishughulisha na biashara za vyakula.

"Mimi sasa hivi nina uwezo wa kuuza 'vi-ndoo' vitatu vya ubwabwa, wakati mwanzo nilikuwa siuzi hata nusu 'ki-ndoo. Wafanyakazi ni wengi kuliko 'Mamantilie'. Nauza juisi ya ukwaju hapa hadi lita 20 kwa siku..."

BIASHARA

KILIMO CHA MWANI TANZANIA BARA ...

# Zao jipya linaloshikiliwa na kinamama, shamba lake ndani bahari mikoa Kusini

## • Kilwa; walimaji kinamama 95%, soko wateja maalumu

**Na Beatrice Philemon, aliyekuwa Kilwa**

**WIKI iliyopita kulikuwapo makala yenye dodoso kuhusu uzalishaji bidhaa mpya ya kilimo, zao la mwani visiwani Zanzibar na mustakabali wa soko lake Je hali ikoje Tanzania Bara? Fuatilia makala ifuatayo na undani wake kutoka Kusini mwa nchi.**

==

Unapozungumzia kilimo cha mwani, inawezekana isieleweke vyema kwa mtu hasa upande wa Tanzania Bara. Ila kwa Zanzibar, inafahamika fika. Kwa ujumla wake ni zao linalolimwa kwenye ukanda wa bahari.

Kimsingi, ni zao linaloota kwenye mazingira tofauti ya bahari, kuanzia kwenye mchanga, matope na mwamba ndani ya bahari.

Kutokana na umuhimu wake kwenye matumizi ya utengenezaji malighafi za viwandani, zao la mwani limekuwa likizalishwa kwa wingi kwenye nchi za Bara Asia na Ufilipino, huku Zanzibar kukiasisiwa mwaka 1993 na baadae kusambazwa hadi Tanzania Bara, mwaka 1996.



Wakulima wa wilayani Kilwa wakikagua bidhaa yao ya Mwani, baada ya kuvuna.

**ILIVYO TANZANIA BARA**

Hadi sasa Tanzania Bara kuna aina mbili za zao la mwani zinazolimwa; Cottonii na Spinosum na kuna wilaya zinazozalisha zao la mwani kwa wingi Tanzania Bara nazo ni Pangani,Mkinga, Bagamoyo, Mafia, Kilwa, Manispaa ya Lindi, Mtama na Mtwara Vijijini.

Mwani unaozalishwa kwa wingi ni Spinosum kutokana na kuhimili hali ya mazingira.

Akizungumzia mnyororo wa thamani wa zao la mwani, Ofisa Uvuvi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, Ahmad Mkali, anasema wilayani humo wanazalisha mwani kama wilaya ilivyo katika nyinginezo zinavyozalisha kwa kiwango kikubwa, ikiwamo mbegu aina za Cottonii na Spinosum.

Hadi sasa kuna vijiji vitano vinavyozalisha; Songosongo, Masoko, Songomnara, Malalani na Kivinje na wilaya ya Kilwa ina uwezo wa kuzalisha wastani wa kilo 600,000 au tani 600 za mwani kwa mwaka, lakini changamoto kubwa bado wakulima wana uhaba wa soko.

Anasema asilimia 95 ya wakulima wa mwani katika wilaya ya Kilwa ni wanawake na kuna jumla ya wakulima 3430 waliojiajiri katika kilimo hicho na uzalishaji mwani ndani ya wilaya upo wa aina mbili, ambazo ni wa mkataba na utaratibu huria.

Kwa upande wa wanunuzi, hadi sasa kuna kampuni mbili zinazonunua mwani kutoka kwa wakulima na kuuza katika bara la Asia katika nchi za Thailand, Ufilipino, China, Ufaransa na Marekani.

**MFUMO WA UZALISHAJI**

Akizungumzia mfumo wa uzalishaji wa mkataba, Mkali anasema: "Mfumo huu wa uzalishaji unajumuisha uingiaji wa mkataba kati ya mwekezaji na mkulima wa mwani chini ya usimamizi wa serikali ya kijiji na baadae mkulima anapewa vifaa kwa ajili ya kuzalisha mwani, kwa makubaliano ya kumuuzia mwekezaji."

Pia, ni mfumo unaompa nafasi mkulima na mwekezaji, wanaingia katika makubaliano ya namna ya kumhudumia mkulima na utaratibu wa kuuza mwani huo anaovuna.

"Utaratibu huu unampa fursa mkulima wa mwani kupata pembejeo za kulimia mwani na mwekezaji anapata uhakika wa kununua mwani kutoka kwa mkulima kwa bei ya soko," anafafanua.

Pia Mkali anaeleza namna kwamba mkulima naye atakuwa na uhakika kupata pembejeo na mwekezaji anakuwa na uhakika kupata mwani, pia uzalishaji unaongezeka.

Mara nyingi, ununuzi wa mwani hufanyika kwa siku maalumu zilizopangwa na ama mwekezaji au mnunuzi na mpaka sasa kilimo cha mkataba kinatekelezwa katika eneo la Masoko Pwani, Songomnara, Pande Plot na Kilwa Kivinje (Mayungiyungi).

Anasema jumla ya wakulima 534 wa mwani katika maeneo hayo wameingia mkataba na kampuni kwa ajili ya kilimo cha mwani, kati ya hao 467 ni wanawake na 67 wanaume.

"Katika eneo la Masoko Pwani kuna wakulima 214, kati ya hao, 194 ni wanawake, 20 wanaume, Songomnara wakulima 80, kati yao wanawake ni 58 na wanaume 22, wakati Pande Plot kuna wakulima 160, kati yao 145 wanawake na 15 wanaume," anasema.

Mkali anaongeza kuwa katika eneo la Kilwa Kivinje (Mayungiyungi) kuna wakulima 80, wanaojumuishwa na kina mama 70 na kaka zao idadi yao iko 10.

Hapo anataja changamoto zinazowakabili katika mfumo huo ni upatikanaji pembejeo ikiwa ni hitaji muhimu kwao, ikizingatiwa wako wengi.



Shamba la Mwani lililoko wilayani Kilwa. **PICHA ZOTE: BEATRICE PHILEMON.**

**WAZALISHAJI HURIA**

Hadi sasa kunatajwa kuwapo wakulima 2,017 katika kijiji cha Songosongo wanaozalisha mwani kwa njia huria, wasio na mkataba na mwekezaji, wao wanajitegemea kwa kila kitu kuanzia pembejeo hadi zao linapotoka shambani. Kati yao, wapo wanawake 1,501 na 516 ni wanaume.

"Mfumo wa uzalishaji huria, huu hauhusishi uingiaji mkataba baina ya mkulima wa mwani na mwekezaji/mnunuzi," anasema.

Chini ya mfumo huo, mkulima anajitegemea kwa vifaa vya kulima na anakuwa huru kuuza mazao yake kwa mnunuzi yeyote na kwa muda wowote. Pia, katika hilo mkulima yuko huru kuuza kwenye soko au mnunuzi ampendaye.

Hata hivyo, ofisa huyo anataja shida ya mfumo huo,ni mkulima anaingia gharama kubwa kununua vifaa vya uzalishaji. Anaendelea kufafanua: "Hii inamaanisha mkulima analazimika kutumia sehemu ya mauzo yake kwa ajili ya kununulia vifaa vya kilimo cha mwani."

**RUZUKU YA WAKULIMA**

Anasema kwa upande wa ruzuku, halmashauri tajwa kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inayowasaidia wakulima hupata vifaa vya kulimia mwani, pia mikopo isiyo na riba ili kuwawezesha kununua vifaa vya kilimo.

Pia, halmashauri zao zinawafundisha utaalamu wa kuanika mwani kwa kutumia turubai na chanja, ili kupata bidhaa zenye viwango bora na inayokubalika katika soko la ndani, pia ikiangalia jinsi ya kutafuta masoko yenye tija.

**VIKUNDI VYA WAKULIMA**

Mkali anasema, Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa inahamasisha wakulima kuunda vikundi na hivi sasa kuna jumla ya vikundi 36 vyenye wanachama 450 watokao katika vijiji vitano, wote wakilima zao mwani. Kila kikundi kina wanachama kuanzia 10 hadi 15.

"Kati ya hivyo, tayari vikundi vitatu vimepata mkopo kutoka Halmashauri (Kilwa) kwa ajili ya kununua pembejeo za kilimo cha mwani, ikiwamo ununuzi wa kamba za kupandia," anasema

Pia, anataja mafanikio ya kuundwa vyama viwili vya ushirika wa zao la mwani katika vijiji vya Songosongo na Masoko na mwaka jana, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitoa msaada wa kamba katika kijiji cha Songosongo, ili kuwasaidia wakulima wa mwani.

Katibu wa Jukwaa la Wanawake linaloitwa "Tumaini Jipya kwa Wanawake Kilwa (TUJIWAKI)', Pili Kuliwa anasema zao la mwani katika wilaya ya Kilwa linalimwa na wenye uwezo mdogo na huwa linalimwa kwenye maji madogo ya bahari na uzalishaji wake ni mwepesi, ukilinganisha na mazao mengine.

Zao hilo analitaja kwamba linawapatia wakulima kipato kwa kuongeza thamani na kutengeneza vitu mbalimbali kama vile sabuni, dawa ya mswaki, mafuta, tambi, dawa ya asili kutibu magonjwa ya mlipuko na bidhaa nyingine.

Pili, analieleza zao la mwani kwamba linalonunulika, lakini lina wateja wachache, hata kusababisha kuitoa nje ya ushindani wa kibiashara.

"Kutokana na changamoto hii, tunaomba biashara hii itangazwe na serikali, ili wawekezaji waje kuwekeza katika zao la mwani kutoa ajira kwa wakazi wa wilaya ya Kilwa, hata kulipandisha thamani zao hili.

"Mwani upo mwingi, lakini hakuna soko. Ndiyo, maana wanunuzi wanaokuja kununua mwani wanapanga bei wenyewe. Hivi sasa mwani unauzwa shilingi 600 hadi 1,500 kwa kilo katika kijiji cha Kivinje," anasema.

Kutokana na tatizo hilo, wakulima wanaomba bei ya kilo moja ya mwani kupanda angalau wastani wa shilingi 2,000 kwa kilo, wakifafanua kuwa bei hii inalipa' ikilinganishwa na uzalishaji wanaofanya.


Pia, anaiomba Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa iwaruhusu wakulima wajipangie bei wenyewe, badala ya wanunuzi kujipangia, au halmashauri iweke bei maalumu itakayomnufaisha mkulima, pia mnunuzi.

Lingine ni kwamba, wakulima wanaiomba halmashauri husika, iwatengee sehemu maalum ya uwazi kama ilivyo kwenye soko la samaki, iwe soko la wakulima kuuzia mwani wao, kwani sasa wanunuzi wanapata shida kuupata mwani, kwa sababu hakuna sehemu maalumu.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Hili la hodi Homa Manjano tusipuuze, umakini jamani!



**NA JENIFER GILLA**
Simu: +255 714 438523
barua pepe:
jenifergilla2@gmail.com

JUZI Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, ametoa tahadhari ya kuzuka ugonjwa wa homa ya manjano au 'Yellow Fever' amesema Machi 3 mwaka huu, Wizara ya Afya ilipokea taarifa kutoka WHO ya kuwapo mlipuko wa ugonjwa wa homa ya manjano, nchini Kenya.

Waziri anasema hadi kufikia tarehe hiyo, Kenya kulikuwa na wagonjwa wa homa ya manjano 15 na vifo vitatu na katika sampuli sita zilizopimwa, maabara ya Kenya kwa kutumia vipimo vya 'serology' na PCR sampuli tatu zilithibitika na maambukizi.

Kutokana na hali hiyo waziri aliwataka wananchi kuchukua tahadhari kwa kuzingatia nchi hizo mbili zimepakana na zina ushirikiano wa mambo mbalimbali, ikiwamo kibiashara.

Waziri aliwataka Watanzania kuzijua na kuzizingatia dalili za ugonjwa wa homa ya manjano kama homa, kuumwa kichwa, maumivu ya misuli na mgongo, mwili kutetemeka, kupoteza hamu ya kula, kichefuchefu na kutapika, mwili kuwa na manjano na kutokwa damu sehemu za wazi.

Katika kuonyesha serikali imejidhatiti kupambana na ugonjwa huo ili usiathiri kufikia kiwango cha UVIKO-19, Waziri Ummy, alisema kuwa serikali itaboresha mifumo ya kutoa vyeti vya kielektroniki vya homa ya manjano mipakani.

Lengo la kufanya hivyo, ni kuzuia udanganyifu unaoweza kufanywa na maofisa kuwapa vyeti watu ambao hawajachoma chanjo hali itakayopelekea kuenea kwa kasi kwa maambukizi ya ugonjwa huo.

Waziri, pia aliagiza hospitali zote za rufani nchini kuwa na huduma za kupima na kutoa chanjo ya homa ya manjano kwa wasafiri na wenye uhitaji, pia ameagiza maofisa wa afya mipakani kuhakikisha wasafiri wanaoingia kutoka nchi zenye maambukizi wanakua na vyeti vya chanjo.

Ingawa Waziri alisema kuwa taarifa ya kipindi cha miezi mitatu iliyopita katika mfumo wa ufuatiliaji wa magonjwa zinaonesha kuwa hakuna taarifa zinazoashiria kuwapo ugonjwa wa homa ya manjano, hii isitufanye kubweteka.

Ikiwa ni siku ya pili leo tangu kutolewa kwa tamko hilo, jamii haionekani kushtushwa na taarifa hizo, pengine ikichukulia kuwa ni ugonjwa usio na madhara makubwa au pengine hautoweza kuingia nchini na kuathiri watu.

Labda niwakumbushe kwamba, homa ya manjano ni ugonjwa mkali wa ini unaosababishwa na kirusi cha homa ya manjano au 'HAV'.

HAV husambazwa kutoka mtu mmoja hadi mtu mwingine kupitia ugusaji wa kinyesi cha watu walioathiriwa, jambo linaloweza kufanyika kwa urahisi ikiwa mtu hataosha mikono yake vizuri. Pia, unaweza kupata homa ya manjano kutoka kwenye chakula, maji, au vitu vyenye HAV.

Kutokana na jinsi inavyoambukizwa, tunaona kwamba ikiwa ugonjwa huo utaingia nchini na kwa kasi hii ya watu kuupuuzia kama vile hakuna tamko lolote la afya lilitolewa hivi karibuni, utaweza kuangamiza wengi.

Tusichukulie ugonjwa huu kirahisi, kwa kuwa pengine upo kabla ya UVIKO-19 na haujawahi kuleta madhara. Tukumbuke kwamba, ulikuwapo hapo mwanzo na serikali ilifanya juhudi kuudhibiti, sasa unarudi tena kupitia nchi jirani. Hatuna budi kuisaidia serikali kuudhibiti.

Serikali haitoweza kuudhibiti ugonjwa huu kama wananchi hatutoiunga mkono, tunapaswa kuhakikisha tunatumia maagizo yaliyotolewa na Wizara ya Afya kujikinga pamoja na kwenda kupata chanjo kwa wale ambao bado.

Si vyema, tukahangaika na ugonjwa wa homa ya manjano, ambao unawezekana kuzuilika, wakati tayari tuna ugonjwa UVIKO-19 unaoendelea kutusumbua sisi na dunia nzima, kwa miaka miwili sasa, kutokana na maumbile ya kirusi chake kujibadilisha kila mara.

Shime kwa kila Mtanzania kupigania uhai wake na wa jirani yake kwa kupambana na maambukizi ya ugonjwa huu kuanzia ngazi ya familia na hata kitaifa.

Pia, ni jukumu la serikali pamoja na wadau wa afya kuhakikisha kuwa wanatoa elimu kwa jamii kuhusu ugonjwa huu mpaka pale itakapojiridhisha kuwa wananchi wameelewa na kufanyia kazi. Kila la heri jamani!

UCHUMI

# Jiji Dodoma kuzaliwa upya kupitia ujenzi barabara Km. 112, kona zote kuungana

- Benki Afrika yamwaga Sh. trilioni kadhaa
- Mkanda mpya ndani, nchi jirani, hadi SA
- Angalizo; kilomita inagharimu Sh. bil. 1.2

**Na Agusta Njoji, DODOMA**




Namna ilivyo sehemu ya ramani ya mradi wa barabara mpya jijini Dodoma, ujenzi utakaokamilika mwaka 2025. **PICHA ZOTE: AGUSTA NJOJI**

MNAMO Februari 9, mwaka huu Rais Samia Suluhu Hassan, ameweka jiwe la msingi la Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Mzunguko wa Nje (Outer Ring Road) katika jiji la Dodoma, yenye urefu wa kilomita 112.3.

Sasa inaangaziwa kuwa mradi wenye faida nyingi, huku Rais Samia akisisitiza: "Mradi huu utakapokamilika utakuza uzalishaji na usafirishaji. Unakwenda kupeleka kwenye soko na bidhaa za viwandani na kufufua masoko ili Tanzania kuzalisha zaidi."

Ni mradi unaoelezwa utafaidisha mikoa jirani ya Singida, Manyara, Morogoro na Iringa, pia ukanda wa Afrika Mashariki na nchi nyinginezo jirani.

Anasema, kutokana na Tanzania kutia saini Itifaki ya Eneo la Biashara Huru ya Ukanda wa Afrika (CFTA), nchi 55 wanachama zilikubaliana barabara hiyo itarahisisha biashara na nchi nyingine za Afrika, ikijumuisha wafanyabiashara wa nchini.

Rais Samia anaitaka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara Mjini (TANROADS), mkandarasi na wasimamizi na ushauri, kufanya jitihada za kuhakikisha ujenzi unakamilika kama mikataba inavyoelekeza, ili kutoa fursa ya maendeleo ya mtu mmoja na taifa.

Mradi huo wa jijini Dodoma unaotarajiwa pia kufungua mlango wa uchumi kitaifa, unatekelezwa kupitia mkopo nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

Rais Samia anasema AfDB imewezesha miradi ya barabara yenye urefu wa kilomita 1,914 na thamani ya Sh. trilioni 2.458 sawa na asilimia 66 au theluthi mbili ya bajeti iliyopo ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Miradi inayofadhiliwa na AfDB ni barabara za Kabingo-Kasulu-Manyovu (Km. 260) ambayo ujenzi unaendelea, huku kuna barabara zilizokamilika; Tabora- Mpanda (km 342), upanuzi wa barabara ya Sakina- Tengeru (Km.14) ili iwe njia nne na njia ya mchepuo Kusini mwa Jiji la Arusha, Km. 42.4.

Nyingine katika orodha ni Mbinga- Mbambabay (Km 66); Singida-Babati-Minjingu (Km 223.5); Arusha -Namanga (Km. 105); Iringa- Dodoma (Km. 260); Namtumbo - Tunduru (Km 190), Maya Maya -Bonga (Km 88), Tunduru-Mangaka- Mtambaswala (Km. 202.5).

Katika kujenga miundombinu nchini mbali na AfDB, zimehusishwa Benki ya Dunia, Shirika la Jaica, Benki ya Exim Korea, Mfuko wa Abu Dhabi, Mfuko wa Kuwait, Benki ya India na shirika la mafuta Opec.

Rais Samia anataja wastani gharama ni Sh. bilioni 1.2 hadi 1.5 kwa kila kilomita moja, huku akifafanua kwamba mbali na midaa na mikopo ya kigeni, serikali inatumia fedha za ndani kujenga barabara zaidi ya 23 nchini.

Anasema AfDB imekuwa rafiki wa Tanzania kufadhili miradi mbalimbali ikiwamo ya usambazaji umeme, majisafi na salama na kilimo.

**WAZIRI UJENZI**

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, anasema ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje wa jiji Dodoma, utachochea maendeleo na kuzalisha fursa nyingi za uchumi na biashara.

Mbarawa, anasema pia itapunguza msongamano jijini na itaongeza usafirishaji watu na bidhaa, uzalishaji nao kupanuka, kuboresha mandhari na kuimarisha utalii.

Anasema ni barabara itakayounganisha ushoroba kati ya nchi jirani zikiwamo Kenya, Uganda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na Malawi.

Waziri Mbarawa anafafanua ilivyo barabara hiyo, itakuwa umbali wa kilomita 20 kutoka kati ya jiji, njia nne, ikiwa na taa na maeneo ya kupanda miti kuboresha mazingira.

Aidha, kutakuwapo hamasa nyinginezo barabarani, zikiwamo kiunganishi hadi kati ya jiji urefu wa kilomita 28, vituo vya afya vinne, kuchimba visima vinne na kukarabati shule moja.

**WADAU MRADI**

Mbunge wa Dodoma, Anthony Mavunde, anasema barabara hiyo ni ndefu sana katika ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara, ikizidiwa na tatu zilizoko Afrika Kusini.

Mavunde pia ni Naibu Waziri wa Kilimo, anaitaja kuwa barabara itakayoing'arisha Dodoma, kwa kuongeza urefu wa mtandao wa barabara za lami nchini.

Anaeleza eneo la Veyula kutajengwa kituo cha afya, pia kisima kirefu; Nala kutajengwa kituo cha afya na kisima kirefu, pia kupewa gari la wagonjwa na kuchimbwa kisima.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS) Rogatus Mativila, anasema barabara hiyo itakuwa na maeneo ya mzunguko kila zinapokutana na barabara kubwa kutoka Iringa, Singida, Arusha na Morogoro.

Mhandisi Mativila anataja maeneo muhimu zitakapopita jijini humo ni Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na Ihumwa, kwenye Bandari Kavu itakayotumika na Reli ya Kisasa (SGR) kuhifadhi mizigo.

Pia barabara itajengwa kwa kugawanywa katika vipande viwili; kimoja kilometa 52.3 kati ya Nala-Ihumwa na kingine kilomita 60, kati ya Ihumwa na Nala. Ujenzi huo unatarajiwa kukamilika mwaka 2025.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, anawataka wakazi wake kuchangamkia fursa ya ujenzi na nyingine nyingi jijini humo, wawekeze kwa kushirikiana na sekta binafsi.

**KUTOKA RAIS AfDB**

Rais Samia anasema amezungumza na Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dk. Akinwumi Adesina, ambaye amekubali ombi lake kutaka afadhili miradi mingine na akakubali kuunga mkono uwekezaji nchini, dira ni kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Dk. Adesina ameahidi kuendelea kuwekeza nchini kwa kusaidia kuwezesha wananchi hasa wafanyabiashara wadogo, kinamama na vijana na kuisaidia serikali kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 nchini.

Tangu alipoteuliwa kushika nafasi hiyo miaka sita iliyopita, inaelezwa misaada kwa Tanzania imekuwa ikiongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 1.5 hadi kufikia Dola bilioni 2.5 kupitia miradi mbalimbali.

Anasema, benki hiyo itaendelea kusaidia kuhakikisha maendeleo yanapatikana na kufanikisha mkakati wa kuunganisha Tanzania na nchi jirani kama Rwanda, Burundi, DRC, Kenya, Uganda, Malawi na Msumbiji.

Benki hiyo kihistoria inatajwa imekuwa mshiriki wa maendeleo ya Tanzania na Dk. Adesina akamhakikishia Rais Samia, kwamba wakati wote akiwa rafiki atapata msaada, ili urais wake uboreke.







# Tume Haki za Binadamu yampongeza Rais Samia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, imewapongeza Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Hussen Ali Mwinyi, kwa kuendelea kusimamia haki za binadamu na misingi ya Utawala bora.

Kamishna wa Haki za Binadamu na Utawala Bora, Dk. Fatma Khalfan, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutoa msaada wa magodoro na mzani wa kupimia watoto katika Zahanati ya Ihumwa jijini hapa ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani iliyofanyika juzi.

Alisema, Tume hiyo inawapongeza viongozi hao kwa kuendelea kusimamia na kulinda haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Kamishna alisema moja kati ya kazi ya Tume hiyo ni kuelimisha, kusimamia, kutafiti na kufanya uchunguzi katika maeneo mbalimbali ili kubaini kama haki za binadamu zinafuatwa na misingi ya utawala bora inafuatwa.

Akizungumzia kuhusu msaada huo, alisema wamekuwa na utaratibu wa kufanya shughuli mbalimbali ikiwamo utoaji wa misaada kwa watu wenye uhitaji katika siku ya wanawake.

"Tumekuwa tukiadhimisha siku ya wanawake duniani kwa kufanya shughuli mbalimbali ikiwemo kuongea na wanafunzi pamoja na kutoa misaada kwa vituo vya watoto yatima na wenye uhitaji," alisema.

Alisema lengo la kuongea na wanafunzi imekuwa ni kuwakumbusha kuzingatia masuala ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

"Mpaka sasa tumeanzisha klabu 256 za wanafunzi katika shule mbalimbali nchini lengo ni kuwajengea uwezo wanafunzi kuhusu haki za binadamu na kuepukana na mila potofu," alisema.

Akizungumzia kuhusu msaada huo alisema ni sehemu ya kuunga jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali katika kuboresha miundombinu katika sekta za afya.

"Tunajua serikali inaboresha huduma za afya ili kutoa haki kwa kila mtu kuishi, lakini sisi leo Tume tumetoa msaada wa magodoro pamoja na mzani kwa ajili ya kupimia watoto vyote vikiwa na thamani ya Shilingi milioni moja," alisema.

Akizungumzia hali ya haki za binadamu na misingi ya utawala nchini, alisema ni nzuri ikilinganishwa na maeneo yote duniani.

"Hivi sasa mifumo mbalimbali imeimarishwa ya kuwezesha wanawake kiuchumi," alisema.

Ofisa Muuguzi wa Zahanati hiyo, Tabitha Nyansika, alishukuru kwa msaada huo na kueleza kuwa kulikuwa na uhaba wa magodoro kwenye zahanati hiyo na kusababisha wajawazito kupata wakati mgumu pale wanapojifungua.

"Walikuwa wanajifungua kwa kupokezana sasa unakuta wakati fulani inatokea wanakwenda kwa pamoja hivyo inabidi uwaruhusu kurudi nyumbani kabla muda wa kitaalamu wa saa 24 hadi 48 ili kutoa nafasi kwa wengine kujifungua," alisema Nyansika..



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (katikati aliyeinama), akikagua wadudu waharibifu wa mazao aina ya viwavijeshi, alipofanya ziara ya kutembelea mashamba ya mahindi, katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: RENATHA MSUNGU.**

# Bodi PSPTB yapewa meno kuchukulia hatua wataalamu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeitaka Bodi ya Wataalamu wa Ugavi na Ununuzi Tanzania (PSPTB) kuwachukulia hatua wataalamu wanaokiuka miiko ya kazi yao kutokana na asilimia 70 ya fedha zake kuelekezwa kwenye ununuzi.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru, alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akizindua Bodi ya Wakurugenzi ya PSPTB jijini hapa.

Alisema bado kuna wataalamu wanaokiuka maadili ya taaluma zao na kuitaka Bodi kuchukua hatua.

"Mchukue hatua ili kuzingatia miiko na maadili yao ili kuweka nidhamu kwenye utendaji kazi, nina matumaini mtatusaidia kwenye hili, hiki ni chombo cha kitaaluma tunategemea mtusaidie, ili kuepuka vitendo vinavyofedhehesha serikali," alisema.

Aliahidi kuwa serikali itatoa ushirikiano wa kuondoa vitendo vya ukiukwaji wa ununuzi na ugavi kutokana na fedha nyingi kutumika kupitia taaluma hiyo.

Aliagiza Maofisa Masuhuri wote wa serikali kuzingatia waraka wa ununuzi huku ikiwataka waajiri kutoa taarifa ya ukiukwaji wa maadili ya wataalamu ili hatua stahiki zichukuliwe.

Alisema wana matarajio makubwa wataalam wanaotengenezwa na bodi hiyo, wasiwe wataalam wa kupata vyeti bali wasaidie serikali kwa upana wake ili kupata thamani ya fedha kwenye matumizi yake.

"Hili ni jambo la muhimu matarajio ni makubwa serikali kwa ujumla wake pamoja na jitihada zilizofanyika za kuweka miundombinu, sheria na taratibu za manunuzi, katika kila shilingi moja ambayo watu wanatumia kwenye sekta binafsi, serikalini inatumika shilingi mbili," alisema.

Alisema ununuzi wa serikali ni asilimia 70 ya bajeti.

"Bajeti tunayotekeleza sasa ya takribani Sh. trilioni 36 ukifanya asilimia 70 ni kama Sh. trilioni 25, sasa hizo zote ni ununuzi, zingekuwa zipo sekta binafsi pengine zingeweza kutumika chini ya hapo asilimia 20 hadi 30 na pengine hadi 50, changamoto ninayowapa nyinyi kwa ujumla wenu ni namna gani mtaisaidia serikali kupunguza upotevu au value attraction ambayo ipo loaded kwenye matumizi ili itumike kwenye maeneo mengine ambayo ni productive na kuna wajibu wa kufanya," alisema.

Alisema ikiwezekana kupunguza asilimia 20 ya fedha za manunuzi sawa na Sh. trilioni tano kwa bajeti ya sasa itasaidia kwenye miradi mingine ya maendeleo.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa PSPTB, Godfrey Mbanyi, alisema "Tutaendelea kuchukua hatua kwa wataalamu wetu ambao kiutendaji wanakiuka mienendo, na maadili ambayo waliapishwa, hivi karibuni tulichukua hatua kwa Wakuu wa vitengo vya ununuzi 19 ambao kwenye ripoti ya PPRA walionekana wamefanya vibaya sana kwenye ununuzi."

Alisema kwa miaka miwili iliyopita wamepitia wakati mgumu kiutendaji kutokana na kutokuwa na Bodi hiyo.

"Kuna kipindi tulimkaribisha Waziri Mkuu nilitaka kulia mbele yake, nilimwambia wazi Waziri Mkuu kuwa ukitaka kunipima leo kwa kipimo cha makusanyo utanitumbua kwa sababu ya kutokuwa na Bodi ya Wakurugenzi mapato ya taasisi yalishuka kabisa na kufikia sifuri."

"Kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka saba tulikuja Wizarani kulia kuomba fedha kitu ambacho hakijawahi kutokea tangu tusitishiwe fedha za matumizi ya ofisi Mwaka 2016, unaweza kuelewa umuhimu wa bodi kwa taasisi yetu tunaahidi kufanya kazi kwa weledi,"alisema.

Naye, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Jacob Kibona, aliahidi Bodi hiyo itasimamia na kuimarisha taaluma ya ununuzi na ugavi na kupambana na vitendo vinavyokinzana na maadili ili kuwa na wataalam waadilifu wanaosimamia zaidi ya asilimia 70 ya bajeti ya serikali inayoelekezwa kwenye manunuzi.

Alitaja baadhi ya mambo yanayolengwa kutekelezwa kwenye mpango mkakati wa kuanzia mwaka 2021/22 hadi 2025/26 kuwa ni kukamilisha utafiti wa kitaalamu ambao ulikuwa umesimama, kuandaa ajenda za utafiti ambazo zitatumiwa na wataalam kufanya utafiti wa kisayansi na kuishauri serikali juu ya kuboresha taaluma hiyo.

# Ekari 195 mashamba ya bangi, mirungi zateketezwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

JUMLA ya ekari 195 za mashamba ya bangi na mirungi zimeteketezwa Wilaya ya Rufiji, mkoani Pwani kwa kipindi cha mwaka mmoja cha uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Balozi Dk. Pindi Chana, aliyasema hayo jana alipokuwa akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jijini hapa kuhusu mafanikio ya Rais Samia.

Alisema mashamba ya bangi ni ekari 185 huku mirungi ni ekari 10 zilizoteketezwa kwenye wilaya hiyo.

Alisema katika kipindi hicho kilo 35,227.5 za dawa za kulevya zilikamatwa na kilo 1124.52 za heroin, gramu 811.3 cocaine, kilo 22,741.10 morphine, na kilo 428.60 za methamphetamine.

Alisema kati ya dawa hizo kilo 859.36 zilikamatwa siku moja kwa watuhumiwa saba raia wa Iran na kuvunja rekodi kwa ukamataji huo kuwa wa kwanza wa kilo nyingi tangu nchi ipate uhuru.

Dk. Pindi alisema kuwa kutokana na kero ya mapambano hayo dhidi ya dawa hizo serikali imeanzisha kliniki 15 za kuwahudumia waraibu wa dawa hizo 10,600 kila siku huku ikisimamia upatikanaji wa uhakika wa dawa ya methadone kwa ajili ya tiba ya waraibu wa heroin.

"Kliniki sita za tiba ya methadone zimeanzishwa ambapo Kliniki moja ipo mkoani Songwe katika mji wa Tunduma, Arusha moja na nne zipo jijini Dar es Salaam katika maeneo ya Tegeta, Segerea, Mbagala na Kigamboni. uanzishwaji wa kliniki hizo kunafanya jumla ya kliniki 15," alisema.

Kuhusu miradi, alisema serikali imepata ufadhili kutoka Serikali ya Marekani wa takribani Dola za Kimarekani zaidi ya milioni 700 kwa ajili ya utekelezaji wa programu kukabiliana na Virusi Vya UKIMWI (VVU), Ukimwi, kifua kikuu na malaria.

Alisema kuwa programu hiyo itaendeleza mapambano dhidi ya maambukizi ya UVIKO-19 pamoja na uboreshaji wa mifumo ya utoaji huduma za afya kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi 2023.

Kadhalika, alisema katika kudhibiti athari za VVU na UKIMWI nchini, kwa kipindi hicho kiwango cha unyanyapaa katika jamii kimeshuka kutoka asilimia 28 mwaka 2013 hadi asilimia 5.5 mwaka 2021.

"Kupungua kwa vifo vitokanavyo na UKIMWI kwa asilimia 50 ambapo vifo vimepungua kutoka 64,000 mwaka 2010 hadi 32,000 mwaka 2021. Aidha, kupungua kwa kiwango cha maambukizi mapya ya VVU kwenye jamii ikiwamo maambukizi mapya kutoka kwa Mama kwenda kwa mtoto kushuka kutoka asilimia 18 mwaka 2010 hadi asilimia saba mwaka 2021," alisema.

Pia, alisema Tanzania ipo kwenye hatua nzuri za kufikia malengo ya kidunia ya Tisini Tatu (90-90-90-) mwaka 2020 na Tisini na Tano Tatu (95-95-95) mwaka 2025 ambapo hadi sasa WAVIU (Watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi) wanaofahamu hali zao za mambukizi ni asilimia 83, WAVIU wanaofahamu hali zao za mambukizi na wapo kwenye matibabu ni asilimia 98 na WAVIU waliopo kwenye matibabu na wamefubaza VVU ni asilimia 92.





# Operesheni ukaguzi magari yenye vioo vyeusi yaanza

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limetangaza kuanza operesheni maalumu ya kukagua magari yote ya watu binafsi yaliyowekwa vioo vyeusi ambavyo havionyeshi ndani kwa madai kuwa limebaini kuwa yanafanya kazi ya kubeba bidhaa za magendo.

Kwa mujibu wa Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alipozungumza na waandishi wa habari juzi, katika operesheni mbalimbali walizozifanya asilimia kubwa magari ya watu binafsi yenye vioo vyeusi ndiyo yaliyokamatwa.

Alisema Jeshi la Polisi limejipanga kuanza ukaguzi wa magari hayo na kuwaomba watumiaji wa magari hayo kutii agizo hilo kwa kuwa lina lengo la kukomesha biashara za magendo.

"Katika operesheni zetu mara kwa mara tumekuwa tukikamata magari mengi madogo ambayo yana vioo vyenye tinted yakisafirisha bidhaa za magendo sasa katika kukabiliana na biashara hizo ambazo zina lengo la kukwepa ushuru, lakini kuwauzia wananchi bidhaa zenye viambata sumu tumeanza ukaguzi," alisema Kamanda Matei.

Katika hatua nyingine aliwataka watumiaji wa vyombo vya moto hususani magari madogo kuacha tabia ya kutumia vyombo hivyo kusafirisha bidhaa za magendo na ikibainika polisi watalitaifisha.

Katika hatua nyingine jeshi hilo linamshikilia Abdul Mwakalinga, dereva teksi ambaye ni mkazi wa Uyole (27) akiwa na bidhaa zilizopigwa marufuku kuingizwa nchini pamoja na kutolipiwa ushuru zikitoka nchini jirani ya Zambia.

Mwakalinga alikamatwa majira ya saa 12 jioni Machi 6, mwaka huu baada ya kufanya msako katika Mtaa wa Mwanyanje, ikiwamo vitenge jora 87, nyavu za kuvulia samaki matundu madogo viroba 10, boksi sita zenye vipodozi vyenye viambata sumu aina ya maji ya citrolight.

Vile vile, limemkamata Emanuel Msigala (42), mkazi wa Uyole Mbeya akiwa amepakia na kusafirisha vipodozi vyenye viambata sumu vilivyopigwa marufuku nchini aina ya Coco Pulp kopo 90 kwenye gari yenye namba za usajili T.512 DCS aina ya Toyota Hilux Surf.

Mtuhumiwa huyo ni mnunuzi, msafirishaji na muuzaji wa bidhaa hizo baada ya kufanyika.

Kamanda Matei alisema bidhaa zote zilizokamatwa zina thamani zaidi ya Shilingi milioni tisa na mali hizo zitataifishwa pamoja na watuhumiwa wote wawili kufikishwa mahakamani.



Meneja wa Taasisi ya Tulia Trust ya jijini Mbeya, Jackline Boaz (kulia), akikabidhi ufunguo wa pikipiki kwa Mwenyekiti wa Kikundi cha Uyole, Frank Daud (kushoto) juzi, ikiwa ni mwendelezo wa utoaji wa mikopo ya 'bodaboda', kwa vijana ili kujikwamua kiuchumi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wakulima parachichi watakiwa kusajili AMCOS

Na Grace Mwakalinga, RUNGWE

MKUU wa Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya, Dk. Vicent Anney, ametoa muda wa wiki moja kwa wakulima wote wa parachichi, kuunda na kusajili AMCOS ili kuepukana na ulanguzi unaofanywa na wanunuzi wa zao hilo.

Dk. Anney alitoa agizo hilo jana alipozungumza na wakulima, viongozi wa AMCOS na wanunuzi wa parachichi ambapo katika kikao na wadau hao alipokea malalamiko kwamba kumeibuka wimbi la walanguzi katika zao hilo na kusababisha wakulima kuuza parachichi zao kwa bei ya chini.

Alisema baadhi ya wanunuzi ni walanguzi na utaratibu mzuri wa kuwasaidia wakulima ni kujiunga kwenye Amcos ili kupanga na kuuza mazao yao kwa bei ya pamoja baada ya kukubaliana.

"Nimekuwa nikipokea malalamiko ya mara kwa mara kutoka kwa wakulima wakisema bei ya parachichi sio nzuri hivyo wanaiomba serikali kuingilia kati huku wakilalamikia wanunuzi wa zao hilo kuwalazimisha wakulima baada ya kuchuma wayasafirishe hadi kwenye vituo vyao vya kukusanyia parachichi," alisema Dk. Anney.

Alikemea tabia ya baadhi ya wanunuzi kununua parachichi chini ya bei elekezi ambayo ni Sh. 1600 kwa kilo moja na kuonya atakayebainika atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria na kufutiwa leseni yake.

"Pamoja na mambo mengine, lakini nawashauri wakulima kuanzisha vikundi vitakavyojikita kuanzisha viwanda vya kuchakata zao la parachichi ili thamani ya zao hilo ikiwamo kutengeneza mafuta ya kula, blue band na mafuta ya kupakaa," alisema Dk. Anney.

Baadhi ya wakulima wa Rungwe akiwamo Emmanuel Mwanjejele wa Kata ya Ibigi, alisema anakerwa na tabia ya wanunuzi kuwalazimisha kusafirisha parachichi wao wenyewe baada ya kuvuna.

Alisema utaratibu huo sio mzuri na kuiomba serikali kuingilia kati kwa kutoa waraka ambao utawaelekeza wanunuzi wote kubeba mazao shambani bila kuwalazimisha wakulima.

Katika kipindi hiki cha mavuno Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imefanikiwa kuvuna tani 200 za zao la parachichi na kusafirishwa kuelekea nchi mbalimbali duniani.

# Taasisi ya Tulia yatoa mkopo wa bodaboda nane

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

TAASISI ya Tulia Trust inayomilikiwa na Spika wa Bunge wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson Mwansasu ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Mbeya mjini, imekabidhi mkopo wa bodaboda nane zenye thamani zaidi ya Sh. milioni 20 kwa kikundi cha bodaboda Kanda ya Uyole jijini Mbeya.

Akikabidhi mkopo huo jana, Meneja wa Taasisi hiyo, Jacqueline Boaz, alisema lengo la mikopo hiyo ni kuwawezesha vijana kujikwamua na umaskini kwa kupewa vitendea kazi ambavyo vitawawezesha kujikwamua kiuchumi.

Boaz alisema mkopo huo wa bodaboda kwa Kikundi cha Uyole ni wa awamu ya pili, awali walipatiwa bodaboda 10 na sasa wameongezewa nyingine 10 na kufikia 20.

"Tunatambua mchango wa vijana wanaojihusisha na shughuli za bodaboda hapa jijini Mbeya licha ya kuwasaidia kukuza uchumi wao lakini wamekuwa bega kwa bega kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Mbunge wao Dk. Tulia," alisema Boaz.

Aidha, alisema kikundi cha Uyole kimekuwa na marejesho mazuri ya mikopo tangu kuanza kunufaika kutokana na kila mmoja wao analipa kulingana na makubaliano.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa kikundi hicho, Frank Daud, mbali ya kushukuru kupata mkopo aliahidi kurejesha kwa wakati ili kutoa fursa kwa wengine kukopa.

Alisema mkopo huo umemsaidia kukidhi mahitaji ya familia yake ikiwamo kusomesha na kujenga nyumba ya kifahari.

Naye Fredrick Nsemwa ambaye ni Makamu Mwenyekiti alisema mkopo huo umekuwa na tija kwao kwani mbali ya mradi huo pia hujihusisha na kilimo hivyo wana imani watapiga hatua zaidi kiuchumi.

Miongoni mwa wanakikundi hicho, David Merere alisema Dk. Tulia amekuwa msaada mkubwa katika kuwawezesha vijana kujikwamua kiuchumi kwa kuwakopesha vyombo vya usafiri ikiwamo bajaji na bodaboda ili waweze kuendesha maisha yao.

Merere alisema mikopo hiyo imewasaidia vijana kuwa na kazi nyingi kutafuta fedha za kujikimu na kuachana na tabia mbaya ikiwamo wizi na uvutaji bangi ambazo zinaharibu mwelekeo wa maisha kwa vijana wengi.

Kupitia mikopo inayotolewa na Taasisi ya Tulia Trust imechangia kuzalisha fursa mbalimbali za kwa wakazi wa Jiji la Mbeya miongoni mwa fursa hizo ni wajasiriamali 601 kuwezeshwa Sh. 100,000 ili kukuza shughuli zao.





## Serikali kutoa stahiki bila kuwapo uonevu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema imedhamiria kuwapa stahiki zao wananchi wake bila ya uonevu wa aina yoyote.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alitoa kauli hiyo katika hafla fupi ya kukabidhi hundi ya fidia kwa wananchi wa eneo la (Red Zone) Tunguu ambalo linatarajiwa kujengwa nyumba ya Makamu wa Rais wa Tanzania, hafla iliyofanyika Vuga Mjini Zanzibar.

Alisema katika kadhia iliyokuwa ikiwakabili wananchi hao Serikali ya Tanzania na Zanzibar zimeamua kulisimamia jambo hilo ili wananchi hao walipwe fidia hiyo kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa na vyombo husika.

Hemed aliwapongeza wananchi hao kwa uvumilivu wao na kueleza kuwa hatua hiyo inaonyesha uungwana na uelewa waliokuwa nao na imani kwa Serikali katika kipindi chote ambacho Serikali ilikuwa ikilisimamia jambo hilo.Hemed alitumia fursa hiyo kuwataka wananchi hao kutoa taarifa sehemu husika iwapo itatokea miongoni mwao hajaingiziwa fedha ili taasisi husika ichukue hatua za haraka.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Thabit Idarous Faina, alieleza kuwa miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kumaliza jambo hilo ni pamoja na ushirikishwaji wa taasisi mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali .

Naye Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano, Abdallah Hassan Mitawi, alisema kuwa zoezi la kulipa fidia ni la muda ambapo hatua kadhaa zilichukuliwa kwa lengo la kumaliza malipo kwa wananchi ili kumaliza zoezi hilo.

Akitoa shukrani kwa niaba ya wananchi wenzake, Muhamed Suleiman Khamis, alizishukuru Serikali zote mbili kwa kumalizika kwa zoezi hilo hatua ambayo inaonesha namna Serikali zinavyowajali wananchi wake.

Zaidi ya Sh. bilioni mbili zimekabidhiwa kwa wananchi waliohamishwa eneo la Red Zone Tunguu kupisha ujenzi wa makazi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania , ikiwa ni fidia kwa wenye maeneo hayo.

# Mawaziri waapa, waahidi makubwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, jana aliwaapisha mawaziri 13 na manaibu saba aliowateua.

Walioapishwa ni Jamal Kassim Ali kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Dk. Saada Mkuya Salum kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na Harous Said Suleiman kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Wengine ni Hamza Hassan Juma Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Dk.Khalid Salum Mohammed kuwa Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi, Nassor Ahmed Mazuri kuwa Waziri wa Afya, Riziki Pembe Juma kuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia,Wazee na Watoto na Simai Mohammed Said kuwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale.

Dk. Mwinyi pia aliwaapisha Suleiman Masoud Makame kuwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Rahma Kassim Ali kuwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Lela Mohammed Mussa kuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Shamta Shaame Khamis na Waziri wa Maji Nishati na Madini Shaib Hassan Kaduara.

Kwa upande wa Manaibu Mawaziri walioapishwa ni Juma Makungu Juma kuwa Naibu Waziri Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Hassan Khamis Hafidh kuwa Naibu Waziri wa Afya, Ali Suleiman Ameir kuwa Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Nadir Abdulatif Yussuf kuwa Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Ali Abdulgulam Hussein kuwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Anna Atanas Poul kuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Shaaban Ali Othman kuwa Naibu Waziri wa Maji, Nishati na Madini.

Katika hatua nyingine, Rais Mwinyi alimuapisha Balozi Mohammed Mwinyi Mzale kuwa Kamisha wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Kamishna wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) Yussuf Juma Mwenda.

Wakizungumza baada ya kula viapo hivyo mawaziri na manaibu hao waliahidi kufanya kazi kwa uadilifu na ufanisi ili kurudisha heshima kwa Rais wa Zanzibar kwa kuonyesha imani ya kuwaamini katika kuisaidia nchi, kupiga hatua kubwa ya kimaendeleo.

Dk. Saada Mkuya Salum ambaye ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, alisema Rais Mwinyi amemuamini na kumkabidhi kazi na kuahidi kuhakikisha anatekeleza wajibu wa sheria, kanuni na utaratibu uliokuwepo ili kupeleka mbele maendeleo ya Zanzibar kwa mujibu wa matarajio makubwa waliyonayo wananchi kwa kiongozi wao.

Alisema amepewa dhamana kubwa ya fedha, hivyo hatokuwa tayari kuona wizara yoyote inafanya ubadhirifu wa fedha za umma.

Naye Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Nadir Abdullatif, alisema ni wakati sasa kufanya kazi na kujipanga kwa sababu wizara aliyoteuliwa ina changamoto kubwa ya migogoro ya ardhi.

Hassan Khamis Hafidh, Naibu Waziri wa Afya, alisema atahakikisha anasimamia majukumu na utendaji kwa watumishi wa wizara hiyo ili watumishi wa sekta hiyo kufanyakazi kwa bidii na kuhakikisha wanazipatia ufumbuzi changamoto zote zinazoikabili sekta hiyo ikiwamo ukosefu wa dawa.

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Masoud Makame, alisema mikakati yake katika wizara hiyo ni kuitangaza dhana ya uchumi wa buluu ambayo haijatangazwa vyema.

Kwa upande wao, baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa akiwemo Talib Ali Talib Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi na Peter Agaton Mabwira Makamu Mwenyekiti wa DP Zanzibar, walisema mabadiliko aliyoyafanya Rais Mwinyi ni muhimu kuona watendaji hao wanaendelea kufanya kazi kwa bidii na kujituma zaidi ili kumsaidia kiongozi wao katika kuendesha nchi.

Katika hafla hiyo mawaziri wanne hawakuapishwa kwa sababu katika mabadiliko aliyoyafanya mawaziri hao wanatetea nafasi zao ambao ni Waziri wa Habari, Vijana, Sanaa na Michezo Tabia Maulid Mwita, Masoud Ali Muhammed Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Haroun Ali Suleiman Katiba na Sheria na Utumishi wa Umma na Mudrik Ramadhan Soraga, Waziri wa nchi Ofisi ya Rais,Kazi ,Uchumi na Uwekezaji.




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akikabidhi cheti cha shukrani kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Dk. John Mduma (kulia) kwa kuunga mkono Mkutano Mkuu wa Jukwaa la Wahariri Zanzibar (TEF), uliofanyika katika ukumbi wa Sheikh Idrisa Abdulwakil Kikwajuni Unguja Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# WaterAid yasaidia mtambo kuchakata majitaka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la WaterAid Tanzania lenye makao makuu yake Dar es Salaam, limeikabidhi Serikali ya Zanzibar mtambo wa kuchakata majitaka na kutumika kama njia mbadala kwa ajili ya kilimo.

Mkurugenzi mkazi wa Shirika hilo, Anna Tenga Mzinga, alisema mradi huo umekuja kwa ajili ya kuimarisha mazingira ya usafi na kuwepo kwa matumizi sahihi ya majitaka kwa shughuli za uzalishaji wa umwagiliaji maji mashambani.

Alisema mradi huo umekuja baada ya mwaka 2019 Zanzibar kukabiliwa na mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu ambapo Shirika la WaterAid lilipokea maombi kutoka SMZ kuhusu kuwapo kwa utekelezaji wa mradi wa uchakataji majitaka wenye lengo la kuwasaidia watu wasiokuwa na uwezo kuacha kumwaga ovyo majitaka.

"Mradi huu ambao umegharimu jumla ya Sh.milioni 462 faida zake ni nyingi, ikiwemo kuhifadhi uchafu wa vyoo kuachwa kumwagwa ovyo na kusababisha athari za mlipuko wa maradhi ikiwemo kipindupindu," alisema.

Akizungumza baada ya makabidhiano ya mtambo huo huko Kizimbani Wilaya ya Magharibi A Unguja, Mkuu wa Wilaya hiyo, Suzan Pete Kunambi, alisema uwepo wa mtambo huo utasaidia kuimarisha huduma za usafi wa mji na kuepukana na hatari ya maradhi ya mlipuko yanayoweza kusababisha vifo vya wananchi ikiwemo kipindupindu.

Mkuu wa Wilaya hiyo alisema mradi huo umekuja katika wakati mwafaka ambapo Zanzibar imejipanga katika kuifanya miji yake kuwa safi na kulinda mazingira.

Alisema mradi huo umejikita katika Wilaya ya Magharibi 'A' katika shehia za Mto Pepo na Munduli ambazo mara kwa mara hujitokeza tatizo la mlipuko wa maradhi ikiwemo kipindupindu.

Aliwataka wananchi kuutumia mtambo huo ambao una uwezo wa kuchakata takribani jumla ya tani 10,000 za majitaka kwa siku kwa muda wa miaka 20.

Alifahamisha kuwepo kwa mradi huo unakwenda sambamba na malengo na dhamira ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi kuwa na miji yenye mazingira mazuri ya mifumo ya usafi katika majitaka.

Naye Meya wa Mji wa Zanzibar, Mahmoud Mohd Mussa, alisema kuwepo kwa mtambo wa kuchakata majitaka ni sehemu ya mikakati ya uongozi wa jiji kuona usafi unaimarishwa katika kipindi chote hatua ambayo itakwenda sambamba na mahitaji ya uimarishji sekta ya utalii.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

ELINIOKOA ELIA MACHA anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T 746 CBT – TOYOTA RAV4. Chassis namba SXA110134151. Engine namba 3S9327836. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: ARU/ARU/RB/98906/2022.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Kihonda**
**Wilaya ya Morogoro kituo cha Chamwino**
**Mkoa Wa Morogoro**
**Usimamizi wa Mirathi Na 05…..2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU DAUDI BISMACK URASSA wa MAFIGA MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MIRIAM DAUD URASSA**

### TANGAZO

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 22/03/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 22/02/2022.**

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 35 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late ALEX ELIUTER MLAWA**

**By 1 REMONDA NG'WERINO KOKO.**
**2 . ……………………………….**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 23day of 03 ..2022

Dated at Morogoro this 9 day of 03 ..2022

RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF MPWAPWA AT MPWAPWA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 3/ 2022**
**In the Matter of the Estate of the Late MARIANOELA DANIEL KADUDU**
**And**
**In the matter of Petitioner for letters of administrating by KADUDU MARSHAL KASSIM**
**GENERAL CITATION**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the late Marianoela Daniel Kadudu (Deceased) hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the Petitioner **Kadudu Marshal Kassim**

Objection in the grant should filed on or before the 15 Day of March, 2022

**Dated at Mpwapwa this 01 day of 03, 2022**

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**HATI YA KIAPO**

Mimi **MWANAISHA ABDALAH JUMA,** wa simu 0655 597570 mtu mzima mwenye akili timamu, mkazi wa Mtaa wa kisosora kata ya Chumbageni katika Halmashauri ya Jiji la Tanga, bila kushawishiwa na mtu yeyote naapa kama ifuatavyo:-

1. KWAMBA, mimi MWANAISHA ABDALAH JUMA, ni mmiliki wa Hati ya kiwanja namba Q 15 Kitalu kilichopo Kisosora katika Halmashauri ya Jiji la Tanga.
2. KWAMBA, hati Miliki ya kiwanja hicho imepotea na nimefanya juhudi za kutafuta bila mafanikio.
3. KWAMBA, kwa kiapo hiki naiomba Idara ya Ardhi na Mipango miji wilaya ya Tanga inipatie hati nyingine ya umiliki wa kiwanja hicho.

**UTHIBITISHO**

Mimi MWANAISHA ABDALAH JUMA, nathibitisha kuwa yote niliyoyasema hapo juu kuanzia aya ya 1-3 ni kweli tupu kwa jinsi nijuavyo na kwa mujibu wa sheria ya viapo (The Oaths and Statutory Declaration Act.Cap.34 R; E 2019)

**MBELE YA…..AZIZ KHAMIS**
**CHEO…HAKIMU**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Kihonda**
**Wilaya ya Morogoro**
**Mkoa Wa Morogoro**
**Usimamizi wa Mirathi Na 20…..2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU LAINA OMARY KASINGWA wa Kihonda**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA HAMISSI ALLY MAKULUNGA**

### TANGAZO

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 16/03/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 09/03/2022.**

HAKIMU

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu HAMADI ABUELGASIM IBRAHIMU anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya NISSAN X-TRAIL yenye namba za usajili T 744 DUX. Yenye Engine No: QR20466352A Kwa yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu. Taarifa Polisi: TAN/RB/98161/2022

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

MASYL GENERAL ENTERPRISES anatangaza kupotelewa na kadi tatu za Pikipiki aina ya BOXER zenye namba za usajili MC 236 AGL, MC 232 AGL na MC 240 AGL. yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi DOD/DOD/ RB/96423/2022

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 25 OF 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE HENRY NGUVUMALI LYANDALAH**
**AND**
**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY YUSTINA HENRY LYANDALA**
**GENERAL CITATION**
**(Made Under Rule 75 of Probate Rules,1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above mentioned deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grants should be filed on or before the 11 Day of 4, 2022

Dated at Dodoma this 10TH day of March, 2022

Petitioner
Presented for filing this 16 day of February, 2022
RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 32 OF 2022**
**In the matter of the estate of the late of the late DEO YUSTINE MAGEGELE of Mlezi within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by JOHN YUSTINE MAGEGELE**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 21 Day of 4, 2022

***Dated at Dodoma this 10 day of 3, 2022***

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

CESILIA WILLBARD KAMPICHAHALE ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA RAV 4 YENYE NAMBA ZA USAJILI T 503 DTC KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI SHI/KAH /RB/ 230308/2021


**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Wafungwa miaka 30 wizi wa pikipiki

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Lindi imewahukumu watu wawili wakazi wa mikoa ya Mtwara na Dar es Salaam kutumikia kifungo cha miaka 30 jela kila mmoja baada ya kupatikana na hatia ya wizi wa kutumia nguvu.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi Consolata Singano, baada ya kuridhishwa bila shaka na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Washtakiwa hao ni Haridi Mtauwa (22) mkazi wa Mtwara na Arabi Namaomi (36) wa Mbezi Luisi, Dar es Salaam.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Hakimu Singano aliwauliza washtakiwa iwapo wana jambo la kuishawishi mahakama isiwape adhabu kali ndipo wakaomba waonewe huruma kwa madai kuwa ni wakosaji wa mara ya kwanza na pia wanazo familia zinazowategemea.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Singano alimuuliza Mwanasheria wa Serikali, Godfrey Mramba, iwapo ana kumbukumbu ya makosa ya zamani kwa washtakiwa na kujibu hana.

Hata hivyo, aliiomba mahakama iwape washtakiwa adhabu kali kwa kuwa wizi wa pikipiki umeendelea kushamiri ndani ya mkoa wa Lindi.

Mwanasheria huyo alidai vitendo vya wizi mara nyingi vinarudisha nyuma maendeleo ya watu wengine wanaojitafutia riziki kupitia njia halali.

Hakimu Singano akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 11//2021, alisema amesikia hoja za pande zote lakini kutokana na uzito wa kosa, anawahukumu kutumikia kifungo cha miaka 30 jela kila mmoja.

Awali, ilidaiwa na mwanasheria Mramba kwamba washtakiwa wakiwa wanafahamu wanachokifanya ni kosa, Septemba 7, 2021 katika kijiji cha Mibule, Nachingwea, mkoani Lindi, waliiba pikipiki aina ya Haojue yenye thamani ya Sh. milioni 2.4 mali ya Karim Hilahila.

Mramba alidai washtakiwa walifanya unyang'anyi huo baada ya kumkodi awapeleke kijiji cha Mpiruka kilichoko ndani ya Wilaya ya Nachingwea na walipofika njiani, walimshambulia kwa kumpiga rungu kichwani, kisha alianguka chini na kupoteza fahamu na kupata mwanya wa kuondoka nayo kusikojulikana.

Aliiambia mahakama kuwa pikipiki hiyo ilikamatwa Septemba 9, 2021 Kata ya Mnazi Mmoja katika Manispaa ya Lindi, ikiwa inafanyiwa usafi.

# Miradi 294 yasajiliwa mwaka wa Samia Ikulu

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imesajili miradi ya uwekezaji 294 yenye thamani ya Sh. trilioni 18.75 kwa kipindi cha mwaka moja, itakayotoa ajira kwa Watanzania 62,301.

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumzia mafanikio ya mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan katika sekta hiyo.

Alisema kuwa kupitia Kituo cha Uwekezaji (TIC), wamefanikisha usajili huo ambao haujawahi kutokea nchini tangu Tanganyika ipate uhuru.

"Tangu Machi mwaka jana hadi Februari mwaka huu, serikali ya awamu ya sita imefanikiwa kusajili miradi hiyo. Kiwango hiki ni kukubwa, hakijawahi kuandikishwa na kusajiliwa na TIC tangu taifa letu lipate uhuru," alisema Dk. Kijaji.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2020/21, miradi iliyosajiliwa ilikuwa na Dola za Marekani bilioni moja lakini kwa mwaka mmoja wamesajili ya Dola bilioni nane.

Alisema kuongezeka kwa idadi hiyo ya miradi kunatokana na juhudi za Rais Samia za kuongoza makongamano ya kutangaza vivutio vya uwekezaji yaliyofanyika ndani na nje ya nchi.

Aliwataka Watanzania kuendelea kuwapokea wawekezaji wanaokuja nchini kuwekeza kwenye sekta mbalimbali.

Alitaja mafanikio mengine ni kushiriki maonyesho ya Dubai 2022 ya kongamano la biashara na uwekezaji, ambayo yaliiwezesha Tanzania kutia saini hati za makubaliano 37 na mataifa mengine zenye thamani ya Sh. trilioni 18.5.

Alisema kutia miradi hiyo wanatarajia kuzalisha ajira 214,475 za Watanzania. Kati ya hati hizo, 13 zilisainiwa kati ya serikali kupitia wizara zake na wawekezaji wa mataifa mengine.

Alitaja hati nyingine 23 zilikuwa ni kampuni binafsi za Tanzania na kampuni binafsi za mataifa mengine duniani na hati mmoja ni kati ya serikali za Zanzibar na kampuni nyingine za nje ya nchi katika sekta ya utalii.

"Hii ni dhamira ya Rais Samia katika kushirikisha sekta binafsi katika miradi mbalimbali ya maendeleo na kukuza uchumi wa taifa letu, ndiyo maana akisafiri hawaachi nyuma sekta binafsi," alisema Dk. Kijazi.

Alitaja eneo lingine ambalo serikali imefanikiwa ni kurahisisha vibali vya wageni kwa kufanya marekebisho ya sheria ili kuruhusu wawekezaji kuja na wataalamu 10 badala ya watano kama ilivyokuwa awamu.

Waziri huyo pia alisema wanatoa maombi ya vibali kwa njia ya mtandao, hali iliyorahisisha utoaji vibali kwa wageni na wafanyabishara kutoka nje ya nchi.

Dk. Kijaji alisema eneo lingine ni upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji hekta milioni 1.6 lililotengwa kutoka kwenye maeneo ya wizara na serikali kwa ajili ya uwekezaji.

Alisema wanaendelea kuhakiki hati za umiliki na kuweka miundombinu wezeshi ili kuwekewa miundombinu wezeshi kwa ajili ya uwekezaji.

Alitaja mafanikio mengine ni kuanzishwa kwa dirisha moja la uwekezaji itakalosaidia kupata vibali kwa njia ya mtandao badala la kwenda ofisini.

"Pamoja na hilo tunafanya mpango wa kuanzisha mfumo wa kuhudumia wawekezaji sehemu moja kwa kutumia wataalam wa ndani kwa kutumia Watanzania ili ikikorofisha iweze kurekebishwa kwa urahisi na kuendelea kufanya kazi," alisema.

Waziri huyo alisema mfumo huo utasaidia kuboresha ufanisi wa utendaji kazi na utaunganisha taasisi zaidi ya 12 sehemu moja vinavyohusika na uwekezaji ikiwamo ardhi.

"Mfumo huu utarahisisha upatikanaji wa vibali kutoka wiki mbili na tunakolekea sasa ndani ya saa 24 tutatoa kibali baada ya kujaza fomu zote za vibali," alifafanua.

Alitaja taasisi zitakazounganishwa pamoja ni TIC, BRELA, TRA, Kazi na Ajira na Ardhi na baadaye TBS, TMDA, NEMC, TANESCO na OSHA.

Aidha, Dk. Kijaji alisema wameandaa kongani la viwanda eneo la Kihonda mkoani Morogoro lenye ukubwa wa ekari 45 kwa ajili ya kuzalisha mbegu za mafuta.

Eneo lingine ni kongani la viwanda Kigamboni mkoani Dar es Salaam lenye mita za mraba milioni 2.2, litakalokuwa na viwanda 100 vya nguo, kuunganisha magari na uzalishaji dawa za binadamu litakalozalisha ajira 50,000 na uwekezaji wake ni Dola milioni 400 .




Rais mstaafu Jakaya Kikwete, akimkabidhi tuzo Meneja Mauzo na Masoko ya Kampuni ya SGA Security, Faustina Shoo, baada ya kampuni hiyo kuibuka kidedea miongoni mwa kampuni za ndani zinazotoa huduma katika migodi mbalimbali ya madini nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Fisi ajeruhi mwanafunzi kichwani

**Na Happy Severine,** BARIADI

MWANAFUNZI wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Somanda "A", Halmashauri ya Mji wa Bariadi mkoani Simiyu, Hollo Malugu (14), ameng'atwa na fisi wakati akielekea shuleni na kumjeruhi kichwani.

Tukio hilo lilitokea juzi asubuhi, wakati mtoto huyo akielekea shuleni, huku ikielezwa kuwa akiwa barabarani ghafla fisi huyo alitokea katika milima iliyoko kwenye mtaa huo kisha kumshambulia.

Mganga Mkuu wa halmashauri hiyo, Dk. Judith Ringia, akizungumza na waandishi wa habari amethibitisha kupokelewa kwa mtoto huyo hospitalini humo kwa matibabu.

Dk. Ringia alisema kuwa mtoto huyo amejeruhiwa maeneo ya kichwani, na kwamba fisi huyo alimng'ata na kunyofoa nyama, huku akibainisha kwamba madaktari na wahudumu walifanya jitihada za haraka kumpatia huduma ya kwanza.

"Ni kweli mtoto aliletwa hapa akiwa na hali mbaya na ameng'atwa kichwani na kunyofolewa baadhi ya nyama, alipofikishwa hapa hospitali tulimpatia huduma ya kwanza, lakini imeonekana hali yake kuwa mbaya tumempatia rufani apelekwe Bugando mkoani Mwanza," alisema Dk. Ringia.

Alisema mama mzazi wa mtoto huyo alisema kuwa katika mtaa wao kumekuwapo na fisi wengi ambao wanaotokea kwenye pori la magereza la mjini Bariadi.

"Wakati anaenda shule huyu mwanangu, njiani ndipo akavamiwa na akaanza kupiga kelele, ndipo wananchi ambao nao walikuwa njiani wakajitokea na kumwokoa, lakini tayari alikuwa amemjeruhi sana kichwani na mimi nilimkuta akiwa anamwagika damu," alisema.

Mwananchi aliyemwokoa mtoto huyo, Mahega Mpango, alisema bila yeye mwanafunzi huyo angepoteza maisha kwani fisi alikuwa amemkandamiza chini, huku mtoto huyo akiwa anapiga kelele.

"Baada ya kusikia kelele nikakimbia kumwokoa mtoto, ndipo nikakuta fisi akiwa amemkandamiza mtoto chini, huku akimng'ata kichwani, nikachukua mawe na kuanza kumpiga ndipo akakimbia," alisema Mpango.

"Baada ya tukio hilo, wananchi wa mtaa huo walichukua uamuzi wa kuanza kumfukuza fisi huyo, lakini juhudi zao hazikuzaa matunda kutokana na mnyama huyo kuwakimbia na kutokomea katika msitu wa magereza."

Aidha, wananchi hao wameitaka serikali kupitia Mamlaka ya Wanyamapori kuwasaidia kufanya msako ili kuwafukuza fisi hao.

"Tunaomba msaada wa serikali, mtaa wetu una fisi wengi sana, ikifika saa 12 jioni wanaanza kuja kwenye maeneo yetu wanatoka milimani au asubuhi ni hatari hususani kwa watoto wetu maana wanakuwa wanakwenda kwenye milima," alisema Emmanuel Magige.

HABARI MICHEZO

# POLISI TANZANIA YAANZA KUINOLEA MAKALI SIMBA

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Polisi Tanzania kinatarajia kucheza michezo mitatu ya kirafiki kwa ajili ya kujiimarisha kukabiliana na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, imefahamika.

Polisi Tanzania itaikaribisha Simba katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa Machi 27, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ushirika ulioko Moshi mkoani Kilimanjaro.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Polisi Tanzania, George Mketo, alisema michezo hiyo itasaidia kuwaweka sawa wachezaji wake ili kuwakabili Simba ambao wana 'joto' la mechi za kimataifa.

Mketo alisema wanahitaji wachezaji wao wawe imara na kuhakikisha wanazibakisha nyumbani pointi tatu dhidi ya mabingwa hao mara nne mfululizo.

"Tunatarajia kutafuta michezo mitatu ya kirafiki kabla ya kukutana na Simba, lengo kubwa ni kuzidi kuwaweka sawa wachezaji wangu, tunahitaji kuingia uwanjani tukiwa na morali kubwa," alisema Mketo.

Kocha huyo alisema anaupa umuhimu mkubwa mchezo huo kwa sababu anafahamu mara zote wanapokutana na Simba, mchezo huwa mgumu na wenye ushindani.

Kuhusu hali za wachezaji wake alisema zinaendelea vizuri na kuongeza nyota wote wako kambini na wanaendelea na programu zilizoandaliwa na benchi la ufundi la timu hiyo inayomilikiwa na Jeshi la Polisi hapa nchini.

Kwa upande wa Ofisa Habari wa Polisi Tanzania, Hassan Juma, alisema Kamati ya Utendaji ya klabu hiyo iliyokutana Machi 7, mwaka huu, jijini Dodoma ilitathmini maendeleo ya timu yao kuelekea hatua ya lala salama ya Ligi Kuu Bara.

"Kamati ya Utendaji ya klabu ilikaa na kutathmini maendeleo ya timu yetu, vile vile ilijadili kutoa bonasi kwa wachezaji ili wazidi kupata ari ya kufanya vizuri ikiwamo kuzibakisha pointi tatu za michezo yetu yote ya nyumbani," alisema Hassan.

Polisi Tanzania itashuka dimbani kuikaribisha Simba ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa bao 1-0 walioupata dhidi ya Azam FC.



Mchezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Watu Wenye Ulemavu (Tembo Warriors), Shedrack Hebron (katikati), akiwa na baadhi ya viongozi na ndugu zake kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere kabla ya kusafiri kuelekea Uturuki kujiunga na klabu ya Yeditepe. **PICHA: SAADA AKIDA**

# Nyota Tembo Warriors safi

**Na Saada Akida**

WAKATI bado wachezaji wengine wawili wa Timu ya Soka ya Taifa ya watu wenye ulemavu (Tembo Warriors), wakikwama kuondoka nchini kutokana na kukosa nauli, Shedrack Hebron aliondoka kuelekea Uturuki juzi ili kujiunga na klabu ya Yeditepe ya jijini Istanbul.

Hebron ni mchezaji wa pili baada ya wiki iliyopita mshambuliaji wa timu hiyo, Frank Ngailo kusajiliwa na klabu ya Izmir baada ya kufuzu majaribio yake ndani ya klabu hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Rais wa Chama cha Mchezo wa Watu Wenye Ulemavu Tanzania (TAFF), Peter Sarungi, alisema Tembo Warriors ikijiandaa kwenda katika fainali za Kombe la Dunia, imeendelea kuvuna matunda kwa wachezaji wake kupata nafasi za kwenda kucheza soka la kulipwa.

Sarungi alisema baada ya kufanikiwa kumuuza Ngailo huko Uturuki, wanajisikia faraja kuendelea kutoa nyota wengine kwenda kufanya majaribio nje ya Tanzania na hiyo itasaidia kujenga Tembo Warriors.

"Hebron anakuwa mchezaji wa pili wa Timu ya Taifa kwenda Uturuki baada ya Ngailo kupata usajili katika klabu ya Izmir, hii inatuonyesha tuna nafasi ya wachezaji wetu kwenda kucheza soka la kulipwa nje ya Tanzania, milango imeanza kufunguka," alisema Sarungi.

Aliongeza nafasi wanayopata nyota wao kwenda kucheza soka la kulipwa inawasaidia kuwaongezea uzoefu na hatimaye watafanya vizuri kwenye fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika Oktoba mwaka huu.

## Sailor, Machomane uwanjani Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Black Sailor inatarajia kukutana na Machomane katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa leo mchana kwenye Uwanja wa Amaan visiwani hapa.

Black Sailor inashuka dimbani ikiwa katika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa ligi hiyo baada ya kujikusanyia pointi 26 wakati wapinzani wao, Machomane yenye pointi tisa wakiwa nafasi ya 15.

Kocha Msaidizi wa Black Sailor, Saleh Machupa alisema wamejipanga kufanya vizuri katika mechi hiyo ili wakao kwenye nafasi nzuri katika msimamo wa ligi hiyo.

Machupa alisema mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu wapinzani wao hawako katika nafasi nzuri hivyo wanahitaji kupata pointi tatu na kujinusuru na janga la kushuka daraja.

Alisema licha ya kuwapo katika nafasi ya kuchungulia mstari wa hatari lakini timu yake imeimarika na inacheza kwa hamasa ili kuhakikisha inamaliza msimu ikiwa kwenye nafasi nne za juu.

"Tunaenda kushindana ili tupate alama tatu, najua utakuwa mchezo mgumu kati ya michezo yote tuliyocheza katika mzunguko wa pili, lakini nina imani lengo la kupata alama tatu litatimia," alisema Machupa.

## SHIMMUTA yaita wadau kugombea

**Na Saada Akida**

BARAZA la Michezo la Taifa (BMT) limetoa wito kwa wadau wenye sifa kujitokeza kuwania uongozi katika uchaguzi mkuu wa Shirikisho la Michezo ya Mashirika ya Umma,Taasisi na Makampuni Binafsi (SHIMMUTA), uliopangwa kufanyika Aprili 9, mwaka huu jijini Dodoma.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Uhusiano wa BMT, Frank Mgunga, alisema lengo la kuhamasisha wagombea kujitokeza ni kwa ajili ya kuhitaji maendeleo kwenye michezo ya taasisi hizo.

Mgunga alisema fomu za wagombea zilianza kutolewa jana na mchakato huo utamalizika ifikapo Aprili 5, mwaka huu, huku usaili wa wagombea ukitarajiwa kufanyika Aprili 8, mwaka huu jijini Dodoma.

"Anayechukua fomu ni lazima awe na sifa zifuatazo, awe raia wa Tanzania, umri kuanzia miaka 18, anatokea kwenye taasisi, kampuni, shirika na awe mwanachama hai," alisema Mgunga.

Alitaja nafasi na ada ya kuchukulia fomu kwa nafasi za Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Mweka Hazina na Mweka Hazina Msaidizi watalipia Sh. 200,000 huku wale wanaowania ujumbe watalipia Sh. 100,000 kila mmoja.

## ZISIKUPITE

### RONALDO, WAKALA WATETA

MSHAMBULIAJI wa Manchester United na Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37 amefanya mazungumzo na wakala wake, Jorge Mendes kuhusu hatima yake hapo Old Trafford. ***(Sun)***

### LEWANDOWSKI ATAKIWA

MSHAMBULIAJI wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Poland mwenye umr wa miaka 33, Robert Lewandowski ananyatiwa na Manchester United. ***(Bild)***

### COUTINHO KUTUA VILLA

KOCHA wa Aston Villa, Steven Gerrard, anataka klabu hiyo kutekeleza chaguo lao la kumsajili Philippe Coutinho kwa euro milioni 40. Hata hivyo, Mbrazil huyo amefanya vyema wakati wa uhamisho wake wa mkopo kutoka Barcelona, lazima apunguze mshahara wake wa pauni 480,000 kwa wiki ili kujiunga na klabu hiyo ya Ligi Kuu England. ***(Telegraph)***

### PHILLIPS AKARIBIA VILLA

KLABU ya Aston Villa huenda pia ikamlenga kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips ikiwa Leeds wataondolewa kwenye michuano hiyo. Bodi ya Villa imejadili ununuzi wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. ***(Athletic)***

### DYBALA HAKIJAELEWEKA

KLABU ya Juventus inajiandaa kuamua ikiwa watamrefushia mkataba mshambuliaji wa Argentina, Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 28, au kushinikiza kumrejesha kiungo wa kati wa Ufaransa. ***(Tuttosport)***

### TUCHEL: CHRISTENSE USIONDOKE

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel ametoa wito kwa mlinzi wa Denmark, Andreas Christensen mwenye umri wa miaka 25 kuipuuza Barcelona na kubakia Stamford Bridge. ***(Mirror)***

### SHAW KUBAKIA UNITED

MLINZI wa Timu ya Taifa ya England, Luke Shaw mwenye umri wa miaka 26 anapania kutia saini mkataba mpya na Manchester United. ***(90min)***

### ARSENAL YASAKA MASTRAIKA

ARSENAL imetoa kipaumbele mpango wa kuwasajili washambuliaji wawili na kiungo wa kati mmoja kama sehemu ya kuimarisha kikosi chao msimu huu wa joto. Washikabunduki hao pia huenda wakamnunua winga mpya na mabeki wawili. ***(Standard)***

### CARLOS BEI JUU

KLABU ya Sevilla imeongeza kipengele cha kutolewa kwa Diego Carlos hadi euro milioni 80. Newcastle ilijaribu kumsajili Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 28 Januari, lakini timu hiyo ya Hispania haikuwa tayari kumuuza beki huyo. ***(Goal)***

### KAMARA ANUKIA ATLETICO

ATLETICO Madrid wanaongoza katika mbio za kumsajili kiungo mahiri wa Ufaransa na Marseille, Boubacar Kamara. Manchester United na Newcastle pia wamehusishwa na uhamisho wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Footmercato)***

### GIL KUBAKI VALENCIA

WINGA wa Hispania, Bryan Gil mwenye umri wa miaka 21 anaweza kubakia Valencia msimu ujao baada ya kujiunga na klabu hiyo kwa mkopo akitokea Tottenham Hotspur Januari. ***(Star)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ANCELOTTI AFURAHIA KIWANGO CHA BENZEMA

**Mfaransa huyo afunga hat-trick na kuiondoa PSG huku akiweka rekodi...**

**MADRID, Hispania**

CARLO Ancelotti alimsifia Karim Benzema "kiongozi wa kuvutia" baada ya straika huyo wa Real Madrid kufunga mabao matatu 'hat-trick' na kuiondoa Paris Saint-Germain kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa juzi.

PSG walionekana kama wana nafasi nzuri ya kusonga mbele baada ya Kylian Mbappe kuwaweka mbele kwa uwiano wa mabao 2-0 kipindi cha kwanza, lakini mchezo huo ukamalizika kwa mabao 3-1.

Los Blancos walirudi kwa kasi kipindi cha pili, shukrani kwa mabao matatu ya Benzema kwenye mchezo huo wa pili wa hatua ya 16.

Mabao hayo yalimfanya Benzema kuwa mchezaji kwenye umri mkubwa zaidi kufunga hat-trick kwenye historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya (miaka 34 na siku 80), siku 17 zaidi ya Olivier Giroud aliyefunga Desemba 2020 wakati Chelsea ikicheza dhidi ya Sevilla.

Pia mabao hayo yalimfanya kumzidi Alfredo Di Stefano na kutinga nafasi ya tatu kuwa mfungaji bora wa wakati wote wa Madrid akifikisha mabao 309.

Ancelotti alimsifia sana straika huyo kwa kuiwezesha Madrid kufuzu hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Karim Benzema ni kiongozi anayevutia, mshambuliaji wa kati anayevutia," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Nina furaha kubwa na kile anachofanya pamoja na mtazamo wake.

"Baada ya bao la kwanza, tuliingia kwenye wakati mzuri, tulisukumiza mashambulizi mbele na kutawala mchezo kwa ubora kabisa.

"Tulikuwa na wakati mgumu mara chache zaidi katika kipindi cha pili ikilinganishwa na kipindi cha kwanza."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,013

MECHI KALI
LIVERPOOL
VERSUS
INTER
1 | 1.57
X | 4.31
2 | 5.21

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GERRARD HANA HARAKA KUMSAJILI COUTINHO




**LONDON, England**

KOCHA wa Aston Villa, Steven Gerrard amesema hana haraka ya kumsajili nyota wake ambaye yupo kwa mkopo kwenye klabu hiyo, Philippe Coutinho na kumpa mkataba wa kudumu.

Coutinho amekuwa mchezaji bora katika mchezo ambao Aston Villa walishinda 4-0 dhidi ya Southampton Jumamosi iliyopita.

Na Gerrard alielezea kiwango cha Coutinho na kusema, "kwa sasa kiwango chake ni kama kile cha zamani akiwa Liverpool.

"Kwangu haileti maana kufanya uamuzi wowote kwa sasa, tunahitaji kumfanya afurahie hapa.

"Kumweka sawa mpaka mwisho wa msimu na nina uhakika atatusaidia sana, kumwangalia na kufanya nae kazi na kumwona akirudi kwenye kiwango chake huku akifurahia mpira wake tena."

Kuna taarifa kuwa Aston Villa wamepewa ofa ya kumsajili kwa mkataba wa kudumu mwishoni mwa msimu huu ambapo watapaswa kulipa kiasi cha pauni milioni 33 kama ada yake.

# Xavi: Wachezaji wanaitaka Barca

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernandez, amesema hakuna mchezaji aliyekataa kujiunga na klabu hiyo tangu alipochukua mikoba ya kuinoa baada ya kuulizwa kuhusu kikao chake alichofanya na Erling Haaland.

Xavi hakuweza kuthibitisha wala kukataa kuhusu kikao ambacho alifanya na Haaland nchini Ujerumani, huku akijua Barcelona ni miongoni mwa klabu zinazowania pamoja na Real Madrid na Manchester City.

"Ni uthibitisho au swali? Angalia, mara zote ni vizuri kusajiliwa na Barcelona, kwangu, hii ndio klabu bora duniani, na kiukweli, hakuna hata mchezaji moja ambaye amesema hapana kwa Barcelona tangu niwe hapa kama kocha."



Alipoulizwa ni jinsi gani anawashawishi kuwasajili wachezaji, Xavi aliongezea, "unawaelezea jinsi tunavyocheza na tunavyowafundisha, unawaambia watakugusa mpira mara 40 kwenye mchezo badala ya mara 20.

"Najaribu kuwaacha waijue kuhusu klabu ni jinsi gani jiji lilivyo zuri. Naibadilisha hiyo kuwa nafasi ya dhahabu kwa mchezaji yeyote na aina ya uchezaji ambayo itawafanya wawe bora."

## HABARI MICHEZO


3,643,920

JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 12/03/22 | 18:00 | Millwall vs Middlesbrough | 2.22 | 3.20 | 3.15 |
| 02. 12/03/22 | 18:00 | Coventry vs Sheffield Utd | 2.60 | 3.14 | 2.65 |
| 03. 12/03/22 | 18:00 | Blackpool vs Swansea | 2.36 | 3.29 | 2.85 |
| 04. 12/03/22 | 19:00 | Montpellier vs Nice | 3.02 | 3.47 | 2.24 |
| 05. 12/03/22 | 23:00 | Troyes vs Nantes | 2.63 | 3.22 | 2.68 |
| 06. 12/03/22 | 23:00 | Getafe vs Valencia | 2.46 | 3.06 | 3.06 |
| 07. 12/03/22 | 23:30 | Belenenses vs Boavista | 2.71 | 3.25 | 2.51 |
| 08. 13/03/22 | 14:15 | Fortuna Sittard vs Willem II Tilburg | 2.80 | 3.35 | 2.48 |
| 09. 13/03/22 | 15:00 | Luton Town vs QPR | 2.25 | 3.20 | 3.10 |
| 10. 13/03/22 | 15:30 | Hannover vs Nurnberg | 2.50 | 3.24 | 2.70 |
| 11. 13/03/22 | 17:00 | Angers vs Reims | 2.27 | 3.13 | 3.28 |
| 12. 13/03/22 | 17:00 | Strasbourg vs Monaco | 2.37 | 3.32 | 2.92 |
| 13. 13/03/22 | 17:00 | Everton vs Wolverhampton | 2.29 | 3.26 | 3.16 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 11/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 17:30 | 1045 | Jihlava vs Zbrojovka Brno | 3.85 | 3.37 | 1.84 |
| 17:30 | 2149 | NK Sesvete vs Cibalia Vinkovci | 1.91 | 3.27 | 3.71 |
| 17:30 | 2474 | NK Dugopolje vs Orijent Rijeka | 1.99 | 3.18 | 3.52 |
| 17:30 | 2889 | Naft Masjed Soleyman FC vs Persepolis FC | 8.49 | 3.81 | 1.39 |
| 18:00 | 3825 | JS Saoura vs HB Chelghoum Laid | 1.35 | 4.32 | 7.68 |
| 18:00 | 4266 | Othellos Athienou vs Ermis Aradippou | 4.60 | 3.30 | 1.86 |
| 18:00 | 5545 | Sport Podbrezova vs MSK Namestovo | 1.01 | 12.54 | 43.39 |
| 19:00 | 5562 | Moroka Swallows FC vs Bloemfontein Celtic | 3.13 | 3.04 | 2.22 |
| 20:30 | 1597 | Hansa vs Holstein Kiel | 2.28 | 3.33 | 2.94 |
| 20:30 | 2259 | FC Juniors OO vs Vorwarts Steyr | 2.56 | 3.42 | 2.40 |
| 20:30 | 2397 | SV Darmstadt vs Sandhausen | 1.45 | 4.51 | 5.89 |
| 20:30 | 2844 | Rapid Vienna II vs Blau Weiss Linz | 3.18 | 3.57 | 1.98 |
| 20:30 | 3124 | SV Lafnitz vs Amstetten | 2.28 | 3.46 | 2.69 |
| 20:30 | 5452 | FC Liefering vs Austria Vienna II | 1.52 | 4.24 | 4.82 |
| 21:00 | 1173 | Creteil vs Concarneau | 3.47 | 3.12 | 2.10 |
| 21:00 | 1753 | Avranches vs Chambly | 2.40 | 3.12 | 2.87 |
| 21:00 | 1809 | Sonnenhof Grossaspach vs VfR Aalen | 2.02 | 3.61 | 3.04 |
| 21:00 | 1965 | Sete 34 FC vs Sedan | 2.71 | 2.95 | 2.66 |
| 21:00 | 3181 | Le Mans vs Boulogne | 2.10 | 3.03 | 3.57 |
| 21:00 | 5442 | Cholet vs Red Star | 2.88 | 3.17 | 2.37 |
| 21:30 | 2573 | FC Schaffhausen vs Yverdon-Sport FC | 1.88 | 3.57 | 3.47 |
| 22:00 | 1541 | Cambuur vs Ajax | 12.77 | 8.05 | 1.14 |
| 22:00 | 1633 | Puskas Akademia vs Paksi FC | 2.15 | 3.79 | 2.69 |
| 22:00 | 3381 | Excelsior Virton vs KVC Westerlo | 7.42 | 4.59 | 1.37 |
| 22:00 | 5830 | FC Eindhoven vs VVV Venlo | 1.72 | 3.86 | 4.10 |
| 22:15 | 5794 | FC Winterthur vs FC Aarau | 2.45 | 3.27 | 2.59 |
| 22:25 | 3843 | SKN St Polten vs Floridsdorfer AC | 2.16 | 3.32 | 2.98 |
| 22:30 | 3072 | Gornik Leczna vs Legia Warszawa | 4.05 | 3.14 | 1.87 |
| 22:30 | 4684 | GKS Tychy vs Zaglebie Sosnowiec | 2.08 | 3.28 | 3.18 |
| 22:30 | 5160 | Ingolstadt II vs FC Ismaning | 1.49 | 4.80 | 5.60 |
| 22:30 | 5184 | Parma vs Cittadella | 2.04 | 3.24 | 3.54 |
| 22:45 | 1414 | Waterford Utd vs Wexford Youths | 1.24 | 4.84 | 11.61 |
| 22:45 | 1436 | Cork City vs Cobh Ramblers | 1.33 | 4.62 | 7.69 |
| 22:45 | 2691 | Drogheda Utd vs Sligo Rovers | 3.28 | 3.18 | 2.08 |
| 22:45 | 4497 | Tranmere vs Mansfield | 2.67 | 3.16 | 2.57 |
| 22:45 | 4651 | Shelbourne vs Dundalk FC | 3.18 | 3.18 | 2.12 |
| 22:45 | 4724 | Treaty United vs Longford Town | 2.32 | 3.22 | 2.79 |
| 22:45 | 4839 | Bray Wanderers vs Galway United | 2.67 | 3.20 | 2.42 |
| 22:45 | 4923 | OH Leuven vs Union Saint Gilloise | 4.32 | 3.88 | 1.71 |
| 22:45 | 4988 | Ayr United vs Kilmarnock | 3.27 | 3.32 | 2.09 |
| 22:45 | 5772 | UCD Dublin vs Derry City | 5.58 | 3.75 | 1.53 |
| 22:45 | 5832 | Linfield Belfast vs Crusaders Belfast | 1.88 | 3.32 | 3.75 |
| 23:00 | 1040 | Lille vs St Etienne | 1.70 | 3.73 | 4.78 |
| 23:00 | 1553 | Atletico Madrid vs Cadiz CF | 1.31 | 5.02 | 10.03 |
| 23:00 | 2713 | Sevilla Atletico vs Cornella | 2.42 | 3.09 | 2.76 |
| 23:00 | 3019 | West Bromwich vs Huddersfield | 1.84 | 3.33 | 4.21 |
| 23:00 | 3816 | Shamrock Rovers vs Bohemians FC | 1.45 | 4.03 | 6.15 |
| 23:00 | 3910 | Zaragoza vs Fuenlabrada | 1.82 | 3.28 | 4.41 |
| 23:00 | 5038 | Finn Harps vs St Patricks | 3.04 | 3.09 | 2.23 |
| 23:15 | 5031 | Benfica vs FC Vizela | 1.22 | 6.11 | 10.83 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# WACHEZAJI 13 WALA UMEME LIGI BARA

**Na Adam Fungamwango**

JUMLA ya wachezaji 13 wameonyeshwa kadi nyekundu hadi kufikia raundi ya 17 ya Ligi Kuu Tanzania Bara, huku timu za Kagera Sugar, Namungo na Ruvu Shooting zikitoa wachezaji wawili kila moja.

Ni jumla ya timu 10 ambazo wachezaji wao wamezawadiwa kadi nyekundu, huku sita zikiwa hazina mchezaji ambaye ameonyeshwa kadi hiyo.

Kwa mujibu wa takwimu za Bodi ya Ligi, wachezaji wa Namungo FC, Abdulaziz Makame na Khamisi Halifa ni moja kati ya wachezaji 'waliokula umeme' mpaka sasa, huku timu nyingine zenye nyota wawili wawili ni Ruvu Shooting, Santos Mazengo na Abdulswamad Kassim ambaye anaichezea klabu hiyo kwa mkopo akitokea Simba na wa Kagera Sugar ni Stephen Duah na Hamisi Kiiza.

Wachezaji wengine waliopata kadi nyekundu kwenye ligi hiyo ni Mpoki Mwakenyuke wa Mbeya City, Benedict Jacob (Coastal Union), Joseph Majagi (Mbeya Kwanza), Ismail Gambo (KMC), Juma Ramadhani (Polisi Tanzania), Anuary Jabir (Dodoma Jiji) na Henock Inonga kutoka Simba.

Timu sita zilizobaki ambazo wachezaji wake mpaka sasa hawajaonja uchungu wa kadi nyekundu ni Yanga, Azam FC, Geita Gold, Prisons, Biashara United, na Mtibwa Sugar.

Wakati huo huo, mchezaji Frank Ikobela wa Mbeya City anaongoza kwa kuwa na kadi nyingi za njano hadi raundi ya 17, akiwa na kadi saba.

Wachezaji wenye kadi sita za njano ni Kassim Haruna kutoka Polisi Tanzania na Salmin Hoza wa Dodoma Jiji, huku wenye kadi tano ni George Mpole wa Geita Gold, Salum Kihimbwa (Mtibwa Sugar), Sospeter Bajana (Azam), Salum Salum (Biashara United) na George Makang'a wa Mtibwa Sugar




Mwenyekiti wa Kampuni ya Peter's Daughter Initiative, Doreen Noni (watatu kulia), akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya washiriki wa kikundi cha Jukwaa la Burudani ambao litajulikana kwa jina la Hadithi kwa ajili ya kutoa elimu kupitia maigizo, tamthilia, vichekecho na burudani mbalimbali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Lugalo yaandaa Combat Fiddle

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa klabu ya mchezo wa gofu ya Lugalo wanafungua mwaka 2022 kwa kuandaa mashindano ya Combat Fiddle, yanayotarajiwa kufanyika keshokutwa katika viwanja vya klabu hiyo vilivyoko jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Nahodha wa klabu ya Lugalo, Meja Japhet Masai alisema kalenda ya mwaka huu klabu hiyo imesema mashindano ya Combat Fiddle yatahusisha wanachama na wasiokuwa wanachama wa klabu.

Masai alisema malengo makubwa ya kuandaa mashindano hayo kuwapongeza wachezaji ni maofisa wa kijeshi waliopanda vyeo.

"Hadi sasa wachezaji 50 wamejiandikisha na mchezaji awe mwanachama na asiyekuwa mwanachama anayehitaji kulipia kiingilio cha Sh.10,000 na mchezaji anatakiwa kuja na fimbo tano tu watakazozitumia siku ya mashindano ukilinganisha na mashindano mengine," alisema Masai.

Alisema mashindano hayo yatakuwa na kanuni ya mchezaji hatoingia uwanjani na mabegi zaidi ya fimbo hizo, mavazi wanaume watavaa pensi na wanawake watakuwa na mavazi ya kawaida ya mchezo huo wa gofu.

Masai alisema kwa upande wa wachezaji wa klabu yake wamejipanga kikamilifu kuelekea katika mashindano

Michezo
Ijumaa Machi 11, 2022
Nipashe





## Ancelotti afurahia kiwango cha Benzema




Straika wa Yanga, Heritier Makambo, akijifua kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC utakaochezwa Machi 19, mwaka huu. Yanga pia imepanga kucheza mechi ya hisani dhidi ya Timu ya Taifa ya Somalia itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini. **PICHA: MTANDAO**

## Yanga, KMC yasogezwa

**Na Adam Fungamwango**

MECHI ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Yanga dhidi ya KMC FC iliyopangwa kuchezwa Machi 16, mwaka huu, imesogezwa mbele kwa siku tatu ili kuruhusu marekebisho ya miundombinu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Kuanzia Machi 15 hadi 18, mwaka huu, kutakuwa na marekebisho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, hivyo haitawezekana mchezo huo kufanyika katika muda uliopangwa awali.

Taarifa iliyotolewa jana na Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB), imesema mechi hiyo namba 144 ya mzunguko wa 18 sasa itachezwa Machi 19 kwenye uwanja na muda ule ule uliopangwa awali (saa 1:00 usiku).

Iliongeza kuwa mechi nyingine iliyosogezwa mbele ni kati ya Polisi Tanzania ambayo badala ya Machi 27, mwaka huu, itasubiri kupangiwa siku nyingine kwa ajili ya kupisha mechi za kirafiki zilizo kwenye kalenda ya Shirikisho la Soka Duniani (FIFA).

Wakati huo huo Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi Kuu imeitoza Mbeya City faini ya Sh. milioni moja kwa kosa la baadhi ya wachezaji na viongozi wake kumshambulia mhudumu akiwa na meneja wa Uwanja wa Ilulu, Lindi , tukio lililotokea siku moja kabla ya mchezo namba 117 dhidi ya wenyeji Namungo FC.

Pia kamati hiyo imemfungia miezi mitatu na kumtoza faini ya Sh. 500,000, mchezaji wa Ruvu Shooting, Farid Said kwa kosa la kukataa kupeana mkono na waamuzi na wachezaji wa Prisons, wakati timu hizo mbili zilipokutana.

# MAKALLA: TWENDENI NA SIMBA

## ●●●Asisitiza mashabiki kusahau itikadi zao wakati Berkane ikitua tayari...

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

HUKU wapinzani wa Simba, RS Berkane kutoka Morocco wakiwa wameshawasili nchini, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amewataka wadau wa soka kutoka maeneo mbalimbali kujitokeza kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa keshokutwa ili kuwashangilia wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia katika michuano ya kimataifa.

Simba ambao ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara itawakaribisha RS Berkane katika mchezo wa Kundi D wa mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika kuanzia saa 10:00 jioni.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Makalla alisema anawakaribisha Watanzania na wadau wa soka kujitokeza kushuhudia timu hiyo pekee iliyobakia katika michuano ya kimataifa bila kujali itikadi za timu zao pendwa.

Makalla alisema anaamini Simba itafanya vizuri katika mchezo huo na kuendelea kujiweka kwenye mazingira bora ya kusonga mbele katika michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

"Tumepata fursa ya mashabiki kushuhudia mchezo huo, bila kujali itikadi ya timu zetu pendwa, tujitokeze uwanjani kuisapoti Simba kwa sababu ni timu pekee iliyopo kwenye ramani ya michezo ya kimataifa kwa hapa Tanzania," alisema Makalla.

Kiongozi huyo alisema anafahamu mechi hiyo itakuwa na ushindani lakini anaamini Simba itaendelea kufanya vizuri kwenye uwanja wake wa nyumbani, hivyo mashabiki wajitokeze kwa wingi bila kusahau kuzingatia sheria za mamlaka ya afya kuhusiana na kujikinga na ugonjwa wa Uviko-19.

Naye Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema wanaendelea na maandalizi vizuri na kwa upande wa kikosi chao kipo tayari kwa ajili ya mchezo huo.

Ahmed alisema Kocha, Pablo Franco anasisitiza wachezaji kuhusu umuhimu wa mchezo huo na kuhakikisha wanashinda ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele.

"Silaha zetu ziko kambini na wachezaji wana molari, hali ya kujiamini na kuhakikisha tunafanya vizuri katika mchezo huo kwa kuibuka na ushindi mkubwa na kuongoza kundi letu ni ya kiwango cha juu," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza kwa kuwataka RS Berkane wajipange kutokana na aina ya maandalizi waliyofanya lakini pia kurejea kwa wachezaji wao waliokuwa majeruhi kumekifanya kikosi chao kukamilika na kuwa tayari kwa mapambano.

"Wachezaji wako fiti zaidi kuhakikisha tunafikia malengo ya kushinda mchezo huu wa nyumbani, tumejipanga kuzibakisha pointi hapa hapa, tunaamini hilo litatimia, tuko tayari kwa vita," Ahmed alisema.

Wakati huo huo, RS Berkane ilitua nchini jana mchana tayari kwa mchezo huo wa nne wa hatua hiyo ya makundi.

Winga wa timu hiyo, Tuisila Kisinda, alisema amefurahi kurejea Tanzania kwa mara nyingine na kuongeza amejipanga kufanya vizuri katika mchezo huo.

"Nimejipanga vizuri kukutana na Simba katika mchezo huo kwa sababu ninaifahamu na tayari tumekutana nao katika mchezo uliopita, tunajua ni sehemu gani ya kuwabana," alisema Kisinda.

Alisema amefurahishwa pia kuona mashabiki wa Yanga wamejitokeza kuwapokea na kudai ana amini Yanga bado wana mapenzi na yeye.

Naye Fiston Abdulrazaq alisema hajaona mchezaji yeyote wa Simba wa kumsumbua katika mchezo huo, hivyo anawakaribisha mashabiki wa Yanga kujitokeza kwa wingi uwanjani kuishangilia RS Berkane.

Mechi nyingine ya Kundi D itakayochezwa keshokutwa itakuwa ni kati ya wenyeji Asec Mimosas ya Ivory Coast dhidi ya US Gendarmerie ya Niger.

RS Berkane yenye pointi sita ndio vinara wa kundi hilo wakifuatiwa na Simba yenye pointi nne sawa na US Gendarmerie wakati ASEC Mimosas inaburuza mkia ikiwa na pointi tatu kibindoni.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >